epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Desemba 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581888
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Timu Mbowe, Tundu Lissu zachuana

• **Vigogo** hao kukaa meza moja juzi kwaongeza moto, Lissu kufunguka jambo kwa waandishi wa habari leo... *Endelea ukurasa 3*



Mbowe    Lissu




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, baada ya kuizindua katika Wilaya ya Magharibi "B" Unguja, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 21

## ENRIQUE: PSG BADO IPO HATARINI UEFA



KOCHA wa PSG, Luis Enrique alisifu timu yake baada ya...

## Mwinyi aelekeza timu Dira ya Taifa kukutana na wadau ipate mwelekeo

UKURASA 2

UKURASA WA 2

**Hatima** mshtakiwa kuua na kuchoma mkewe kwa magunia ya mkaa, Februari 26

UKURASA WA 5

**TAWLA:** Kinababa mnaonyanyaswa na wake zenu, tumieni njia hii

UKURASA WA 19

**Al** Bashir amrithi Assad Syria; Iran, USA zashutumiana




UKURASA WA 22

## MBAPPÉ APIGA BAO LA 50 UEFA

# Wakuu nchi jirani waja kuzindua kituo mauzo umeme wa TANESCO kimataifa

UK. 18

**MICHEZO** SIMBA YAMTAKA RUPIA WA SINGIDA BS UK.24 **KATUNI** UK.6



Daladala likisubiri abiria jirani na chemba ya maji ya mvua iliyo wazi, katika eneo la Ukonga Banana, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kusababisha hatari kwa abiria wanaoshuka na kupanda. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Hatima mshtakiwa kuchoma mkewe kwa magunia ya mkaa kujulikana Februari 26

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Februari 26, mwakani, inatarajia kutoa hukumu ya kesi ya mauaji inayomkabili mfanyabiashara Khamis Luwonga (38), anayeshtakiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa.

Hukumu hiyo inatarajiwa kutolewa na Jaji Hamidu Mwanga baada ya kusikiliza mashahidi 14 wa upande wa mashtaka na utetezi. Mahakama pia ilipokea vielelezo mbalimbali, ukiwamo udongo wenye masalia ya mafuta yanayodhaniwa kuwa ni ya mwili wa Naomi.

Wakili wa Serikali Cuthbert Mbilingi alidai jana mbele Jaji Mwanga kwamba hawakufanikiwa kuwasilisha majumuisho ya mwisho kama ilivyoelekezwa na mahakama kwa sababu kompyuta aliyokuwa anatumia ilipata hitilafu.

"Tunaomba tuongezwe muda wa nyongeza hadi Desemba 24, 2024 tutakuwa tushayawasilisha mahakamani," alidai Wakili Mbilingi.

Wakili wa Mshtakiwa, Hilda Mushi alidai wao waliwasilisha majumuisho hayo Desemba 10, mwaka huu, kama walivyopewa amri na mahakama.

Jaji huyo alitoa siku 14 kwa upande wa Jamhuri kuwasilisha majumuisho hayo hadi Desemba 24, mwaka huu wawe wameshafaili na hukumu itasomwa Februari 26 mwakani.

Hata hivyo, mshtakiwa alinyoosha kidole na alipopewa nafasi, akaanza kuulalamikia upande wa Jamhuri kushindwa kuwasilisha mahakamani majumuisho hayo ndani ya siku 14.

"Wala usiwe na wasiwasi, huu hata si ushahidi, ni uchambuzi tu ambao na uhalisia wa hii kesi mahakama inahitaji haya wala usiwe na presha kwa sababu unaweza hata ukakusaidia na wewe pia," alisema Jaji Mwanga.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, Kigamboni alimuua Naomi Marijani.

# Mwinyi aagiza timu Dira Maendeleo 2050 kukusanya maoni kwa wadau

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameiagiza timu kuu ya kitaalamu ya Dira ya Maendeleo ya 2050 kukutana na wadau mbalimbali kuhakikisha kazi ya kupokea maoni inakamilika kikamilifu ili kuwa na dira yenye kubeba maono ya wananchi wote.

Pia Dk. Mwinyi ameziagiza Tume za Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Serikali ya Mapiduzi ya Zanzibar kuhakikisha wanaratibu zoezi la uhakiki kwamba linafanyika kwa ufanisi wa hali ya juu pamoja na kuisambaza rasimu hiyo kwa vyombo mbalimbali na kuweka mfumo halisi wa kupokea maoni.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo visiwani hapa alipozindua Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali za SMT na SMZ akiwamo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi amewaagiza viongozi na wataalamu wote wa serikali zote mbili kutoa ushirikiano kwa timu ya kitaalamu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa kuwa kutoshiriki kwao hakutofanikisha azma ya dira hiyo.

Alisisitiza timu hiyo ya kitaalamu inamfikia kila mwananchi nchini ili kutoa maoni bila kujali tofauti za dini, siasa, jinsia, makundi maalum au eneo mtu analotoka ili ibebe maono yao ya miaka 25 ijayo.

Alisema malengo makuu ya rasimu hiyo ni kuona yamegusa moja kwa moja katika kuboresha maisha ya watu, elimu, afya, ustawi wa amani na haki pamoja na kuwa na dira jumuishi ambayo itamshirikisha kila mwananchi kutoa mchango wake kwa maendeleo ya taifa.

Aliishauri timu hiyo kuweka muktadha wa maendeleo ya taifa katika mwelekeo wa makubaliano au mipango ya kikanda na kimataifa, akitoa mfano "Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki" (EAC) 2050; "Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika" (SADC) 2050; "Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi" (Paris Agreement); "Ajenda ya Maendeleo ya Afrika" (Ajenda 2063); "Doha Programme of Action 2022 - 2023" na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs).

Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliishauri timu hiyo ya kitaalamu kuandaa usimamizi mzuri wa kukusanya maoni ya wadau kwa kuzunguka nchi nzima na kuandaa makongamano na majadiliano na wadau.

Akitaja mafanikio ya Dira ya 2025 ambayo inafikia tamati mwezi Juni 2025, alisema kuwa ni pamoja na kuboresha hali ya maisha ya watu, elimu, uboreshaji wa huduma za afya, kupunguza vifo na kuongezeka wastani wa umri wa kuishi, kuimarika kwa utawala wa kisheria na ukuaji wa uchumi.

Alisema, kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Dira 2025, nchi imekuwa kitovu cha amani na imeshiriki kikamilifu hata katika duru za kimataifa kulinda amani barani Afrika, aliwasisitiza Watanzania kuendelea kulinda amani, utulivu na umoja kama misingi muhimu ya kupata maendeleo ya nchi.

Alisema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zenye utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124, licha ya kuwa bado kilimo hakijawa cha kisasa, lakini wakulima wamefanya kazi kubwa ya kuhakikisha nchi haikabiliwi na njaa.

Akizungumzia ustawi wa elimu alisema kumeshuhudiwa ongezeko kubwa la madarasa, vyuo vikuu na walimu, aidha, udahili wa elimu ya msingi umeongezeka kutoka asilimia 69 kutoka mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 97 mwaka 2022, kuongezeka kwa kiwango cha kumaliza elimu kutoka asilimia 51 mwaka 2000 hadi asilimia 70 mwaka 2022 na kufanikiwa kuondoa pengo kubwa lililokuwapo katika elimu ya msingi na sekondari kati ya watoto wa kike na watoto wa kiume.

Kuhusu uboreshaji wa huduma za afya alisema Dira 2025 ilifanikiwa kupunguza vifo na kuongezeka wastani wa umri wa kuishi, kuimarika kwa hizo kuanzia kwenye vituo vya fya, zahanati, hospitali za wilaya, mikoa, kanda hadi taifa.

Akielezea utawala bora na utawala wa sheria ameeleza kuwa limebaki kuwa kipaumbele kwa taifa licha ya changamoto ndogo ndogo ambazo zimeendelea kushughulikiwa na serikali kwa masilahi mapana ya wananchi ikiwamo kuundwa kwa Tume ili kupendekeza namna ya kuboresha taasisi za haki jinai nchini ikiwa ni njia ya kuendelea kuimarisha zaidi mifumo ya haki jinai na hivyo kudumisha utawala bora na utawala wa sheria.

Kuhusu uchumi alisema umekuwa kwa wastani wa asilimia 6.7 ikiwamo kukua kwa biashara na uwekezaji, kujenga miundombinu muhimu kwa sekta zote ujenzi wa barabara na madaraja makubwa, reli ya kisasa, ukarabati mkubwa wa reli ya kati, bandari, meli, viwanja vya ndege, miundombinu ya mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema uzinduzi wa rasimu ya 2050 ni jambo kubwa lenye mustakabali muhimu kwa Taifa la Tanzania.

Alisema kuwa rasimu hiyo ni ya Watanzania wote na kuahidi timu ya kitaalamu ya dira hiyo kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na uaminifu ili hatimaye kuwa na Dira ya 2050 yenye tija na manufaa kwa Watanzania.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Kitaifa ya Maandalizi ya Dira ya 2050, Prof. Kitila Mkumbo, alisema msingi mkuu wa rasimu hiyo umejikita katika usalama, amani na utulivu na kuwa na uchumi imara.

Dk. Saada Mkuya Salum, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Makamu Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Uongozi ya Kitaifa ya Maandalizi ya Dira 2050, alisema Zanzibar imeshiriki kikamilifu kutoa maoni juu ya rasimu hiyo kwa hatua mbalimbali ikiwamo kuratibu maoni ya wananchi huku kukiwa na ushiriki mkubwa wa wanawake.

Rais Dk. Mwinyi alikabidhi Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaliwa kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watendaji wakuu wa taasisi za umma na binafsi.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms/WhatsApp: +255 677 020 701*
*Email: costomerrelations@guardian.co.tz*

# Wanane mbaroni, yumo mama anayedaiwa kuua mwanawe

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATU wanane wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Morogoro kwa tuhuma mbalimbali, akiwamo mwanamke anayedaiwa kumuua mwanawe, kuiba miundombinu ya umeme na kuharibu miundombinu ya kilimo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio la mauaji ya mtoto Simon Gervas (8), mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Lusange lilitokea Desemba 8 mwaka huu majira ya usiku katika kitongoji cha Lusange, kata ya Mtombozi, wilayani Morogoro.

Akielezea tukio hilo, kamanda huyo alisema mama wa mtoto huyo, Teodory Mkunga (39), anadaiwa alimvamia mtoto wake na kumshambulia sehemu mbalimbali za mwili wake, ikiwamo kichwani na mgongoni kwa kutumia silaha yenye nchi kali, akavuja damu kwa wingi na kusababisha kifo chake.

Kamanda Mkama alisema jeshi hilo linawashikilia watu watatu waliokamatwa katika kijiji cha Mndele, wilayani Mvomero wakihusishwa na tuhuma za kuiba rola tano za nyaya za umeme zenye thamani ya Sh. milioni 57, mali ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO).

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni: Dismas Petro (28), mkazi wa Dar es Salaam ambaye ni fundi umeme; Alawi Evodius (32), mkazi wa Mbagala Dar es Salaam; na Muhoza Bombo (40), mkazi wa Kigamboni ambao walikamatwa maeneo ya mtaa wa Boma, Ilala, jijini Dar es Salaam.

Wengine waliokamatwa ni watuhumiwa watatu wanaodaiwa kuhujumu miundombinu ya kilimo katika eneo la kitongoji cha Msimba, kijiji cha Ilonga, wilayani Kilosa.

Watuhumiwa hao jamii ya wafugaji, wakazi wa Madoto, wilayani Kilosa ni Milligo Komiyani (26), Morunge Rombo (30) na Hamis Lambaingwa (27), wote wanadaiwa kuwa wakiwa na kundi kubwa la mifugo, walikata kwa mkasi uzio wa Shamba la Mbegu la Taifa la Msimba na kufanikiwa kuingiza mifugo ndani ya shamba hilo.

Mwingine aliyekamatwa na polisi ni mtuhumiwa anayedaiwa kuwa sugu wa wizi wa pikipiki, Msilivesta Aloyce, mkazi wa Kilosa Mtendeni, kata ya Mkwatani, wilayani Kilosa.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipanda mti aina ya mfenesi katika moja ya nyumba zilizojengwa kupitia Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma, baada ya kuuzindua mpango huo, eneo la Njedengwa, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Mbowe, Lissu wazua jambo mitandaoni

**Na Restuta James**

KITENDO cha Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe kuonekana hadharani akiwa na Makamu wake, Tundu Lissu, kumeibua shangwe mitandaoni, huku baadhi ya wafuasi wa chama hicho wakiendelea kunyukana.

Nipashe imefuatilia maoni kwenye kurasa za chama hicho na ya makada wenye ushawishi mtandaoni, yakionesha mivutano; baadhi wakitaka Mbowe ang'atuke ili ampishe Lissu, wengine wakimtaka Lissu aache wanachodai "kukivuruga chama".

Baada ya kuwapo tetesi kwamba wawili hao hawaelewani kutokana na kinachodaiwa "mpango wa Lissu kuwania nafasi ya uenyekiti wa CHADEMA katika uchaguzi wa ndani ya chama, juzi Mbowe na Lissu walijitokeza wakiwa pamoja mbele ya waandishi wa habari na kuzungumzia hadharani suala hilo.

Vilevile, barua ya kumhoji Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Iringa Mjini, Frank Nyalusi, kuhusu sababu za kuwaondoa mawakala katika vituo siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliofanyika mwishoni mwa mwezi uliopita, umeongeza mnyukano miongoni mwa makada hao mitandaoni.

Aliyekuwa mgombea wa CHADEMA katika Jimbo la Mbarali, mkoani Mbeya, Liberatus Mwang'ombe, amekosoa barua ya kuhoji uamuzi wa Nyalusi, akiihusisha na msimamo wake wa kumuunga mkono Lissu.

Mwang'ombe alisema kwenye mtandao wa X juzi, kwamba uamuzi wa Nyalusi kuondoa mawakala Novemba 27, ulitokana na wengi wao kuzuiwa kuingia katika vyumba vya kupigia kura kwa madai ya barua zao kukosa mhuri wa moto na waliruhusiwa kuingia vituoni baadaye saa sita mchana.

Barua kwa Nyalusi iliyoandikwa na Baraza la Uongozi Mkoa wa Iringa na kutiwa saini na Katibu wake, Leonard Kurwawijilla, imemtaka ajieleze kwa kuwaondoa mawakala vituoni, kukaidi maagizo ya viongozi wa CHADEMA Iringa na Kanda, kuanzia Katibu, Mwenyekiti wa Mkoa na Mwenyekiti wa Kanda, la kumtaka awarudishe na kuwatangazia wanachama wa chama hicho Jimbo la Iringa wasiende kupiga kura.

Barua hiyo ambayo imewekwa kwenye mitandao ya kijamii, ilieleza kuwa uamuzi wa Nyalusi umekinyima chama hicho nafasi ya kutokujua dosari za uchaguzi huo na hivyo kukinyima uhalali wa kuukosoa, jambo ambalo ni utovu wa nidhamu.

Nyalusi ametakiwa kujieleza ndani ya siku 14 kuanzia Jumatatu ya juma hili alipopewa barua hiyo.

Mwang'ombe alidai kuwa barua hiyo imetokana na uamuzi wake wa kuonesha kumuunga mkono Lissu, kwa kuwa kikao cha tathmini ya uchaguzi Iringa kilikaa Novemba 28, 2024 na kuhoji sababu za barua ya kilichoamuliwa kuandikwa wiki mbili baadaye.

Maoni mengi ya makada na wafuasi wa CHADEMA, yalimkosoa Mwang'ombe huku wengine wakimtaka Nyalusi ajibu barua badala ya kulalamika mtandaoni.

Kada wa CHADEMA, Yeriko Nyerere, aliandika kwenye ukurasa wake wa X kwamba wanachama wa chama hicho wanasubiri kuingia katika uchaguzi ngazi ya taifa, lakini hawatamuunga mkono mgombea "anayekishambulia" chama hicho hadharani na sirini.

"Sisi kama wanachama, yeyote anayetafuta uongozi kwa kuungwa mkono na maadui zetu, CCM, huyo siyo mwenzetu, yeyote anayetafuta uongozi kwa kushambulia viongozi wenzake, huyo siyo mwenzetu! Yeyote anayegeuza mkuki kwetu huyo ni adui!

"Tutapambana naye sawasawa na tunavyoshughulika na ma-CCM, haijalishi ni kiongozi wa kitaifa ama ana heshima gani katika taifa.

"Hatuna chama kingine mbadala nchini, hiki chama lazima tukilinde kwa wivu mkubwa, dola iko kazini kuhakikisha chama kinaanguka na kufutika, uzembe wetu kidogo tu utakigharimu chama chetu! Chama kwanza mtu baadaye," aliandika.

Kada mwingine Martin Maranja, aliposti picha ya Mbowe na Lissu wakiwa kwenye mkutano na waandishi wa habari juzi, ambayo ndani ya saa mbili ilikuwa imetazamwa na watu 13,000 huku ikipata maoni 731.

Baadhi ya watu waliotoa maoni kwenye picha hiyo, walikosoa waliokuwa wanasema "CHADEMA ina mpasuko".

"Kuna wachawi humu kutwa kusema Mbowe na Lissu hawapatani, sasa hii ni nini?" walihoji wachangiaji wengi kwenye mtandao wa X juzi.

Juzi kwenye mkutano na waandishi wa habari, Mbowe aliwajibu wanaomtaka ang'atuke kwenye nafasi ya uenyekiti na kusema watakaomwambia aondoke ni wanachama na watakaomwambia agombee ni wanachama.

"Mimi ninashangaa tu huko mitandaoni, pilipili usiyoila inakuwashia nini?" Mbowe alihoji.

Lissu alisema haogopi maneno ya mtandaoni kwa kuwa anaishi na risasi mwilini, hivyo hana anachoogopa.

Mara kadhaa, Lissu amekaririwa akidai "kumepenyezwa fedha chafu ndani ya CHADEMA" na ndio maana amekuwa akikemea rushwa hadharani.

Mwezi uliopita, Mbowe alisema tofauti ya mitazamo kati yake na Lissu, haina maana kuwapo mpasuko wala ugomvi ndani ya CHADEMA, bali ni uimara wa chama.

"Hatuna ugomvi, hayo ni mambo ya kawaida tu. Ukishakuwa na chama cha siasa kisichokuwa na minyukano, hicho chama ni mfu. Siasa ndivyo ilivyo. Mkiwa kwenye siasa mnakubaliana kila kitu kwa asilimia 100 siku zote, hiyo safari hamtoboi," alisema Mbowe Novemba 19 mwaka huu kwenye mkutano na waandishi wa habari.

Leo Lissu anatarajiwa kuzungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam. Ajenda yake haijawekwa wazi.

# Mvua yabomoa nyumba, yaua

**Na Thobias Mwanakatwe,**

ITIGI

WATU wawili wa familia moja, baba na mtoto wake wamekufa na wengine wawili kujeruhiwa kwa kuangukiwa na nyumba wakiwa wamelala usiku baada ya mvua kunyesha usiku wa kuamkia juzi.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Dk. Vicent Mashinji, akizungumza na waombelezaji jana, alisema tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia juzi saa 7: 00 katika kijiji cha Kashangu Halmashauri ya Itigi, Wilaya ya Manyoni.

Dk. Mashinji aliyeambata na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, alisema serikali imepokea kwa masikitiko tukio hilo na kuwataka wananchi kuanza kujenga nyumba bora za kuishi kuepuka majanga kama hayo hususani kipindi cha mvua za masika.

Aliwataka viongozi wa serikali wa ngazi ya kata na vijiji washirikiane na wazee maarufu katika maeneo yao kuwashauri wananchi kuimarisha makazi yao ili kujikinga na majanga.

"Nitoe rai kwa wananchi kwamba tumetoka kuwa na janga kama hili Dar es Salaam kuna jengo la ghorofa lilidondoka, kwa hiyo majanga haya yanatokea na huku kwetu tuwaombe wazee katika vijiji wanapoona katika maeneo yetu kuna jengo linatia shaka washauri mwenye nyumba na mamlaka za serikali ili kuona namna ya kuepuka majanga," alisema.

Dk. Mashinji aliagiza mamlaka zinazohusika kukagua nyumba kwa kushirikiana na wenyeviti wa vitongoji ambazo zimejengwa kwa matope ili kuona uimara wake.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Dk. Emmanuel Mallage, alithibitisha kupokea miili ya watu wawili waliofariki ambao ni Jeremia Sangalari (66) na Mbalu Jeremia (1).

Dk. Mallage aliwataja majeruhi wanaoendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya kuwa ni Tausi Abubakari (40) na Salumu Jeremia (4).



Baadhi ya wanachama wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, wakifanya usafi mapema wiki hii, kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mahakama yakubali TAKUKURU kumhoji Mkurugenzi JATU

**Na Grace Gurisha**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imekubaliwa na mahakama kufanya mahojiano na aliyekuwa Mkurugenzi wa JATU, Peter Gasaya (33), anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu.

Ombi hilo liliwasilishwa jana na maofisa wa TAKUKURU mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Geofrey Mhini wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakiomba ruhusa hiyo wakati kesi ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Wakili wa Serikali, Roida Mwakamele alidai kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya kutajwa na baadaye maofisa wa TAKUKURU waliwasilisha ombi hilo.

Hakimu Mhini alikubali ombi hilo na kuwataka baada ya kumaliza mahojiano hayo wamrudishe mshtakiwa mahakamani saa 9:00 alasiri ili arudishwe magereza na kuahirisha kesi hiyo hadi Desemba 16, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Mshtakiwa Gasaya anadaiwa kuwa kati ya Januari mosi, 2020 hadi Desemba 31, 2021, jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, alijipatia Sh. 5,139,865,733 kutoka SACCOS ya JATU kwa njia ya udanganyifu.

Ilidaiwa kuwa alijipatia kiasi hicho cha fedha kwa madai ya kuzungusha na kukizalisha kwa kuwekeza katika mazao ya kilimo na kupata faida zaidi, akifahamu si kweli.

Pia anatuhumiwa kutakatisha fedha hizo zilizokuwa katika akaunti ya JATU iliyoko Benki ya NMB Tawi la Temeke, kwa kujirushia katika mitandao ya simu.

Mshtakiwa anadaiwa kufanya hivyo huku akijua fedha hizo zinatokana na kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

# Wami Ruvu yarejesha kilomita 16 mito iliyopoteza mwelekeo

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

OFISI ya Maji Bonde la Wami Ruvu wamefanikiwa kurejesha kilometa 16.1 ya mito iliyopoteza uelekeo wake, katika maeneo mbalimbali kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uharibifu wa mazingira zinazochangiwa na shughuli za kibinadamu zinazofanywa na wananchi.

Mkurugenzi wa Bodi ya Bonde la Wami Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmasy, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kubainisha mito hiyo ni mitano inayopeleka maji yake katika Bwawa la Mindu ikiwamo mto Mlali, Mgera na Lukulunge.

"Nia yetu ni kuhakikisha mito iliyojaa mchanga inarudishwa katika hali yake ya kawaida, tuna changamoto kubwa ya mito yetu kujaa tope na mchanga kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kwenye mteremko mkali na milima hasa kilimo na ufugaji, na mvua ikinyesha mchanga na tope vinaingia kwenye mito, inajaa na kusababisha mito kupoteza uelekeo," alisema Mmasy.

Alisema hali hiyo imesababisha hasara kubwa na mvua ikinyesha mito inakuwa haina kingo na maji yanatawanyika ovyo na kuingia kwenye makazi, mashamba, miundombinu kama ya reli na barabara na kusababisha mafuriko na uharibifu mkubwa.

"Tulichofanya ni kuifukua mito na kupanda magugu pembeni na mwisho wa siku kurudisha katika hali yake ya kawaida na sasa kurejea katika Bwawa la Mindu, lakini pia kwa Mto Ruvu, kuna mito miwili, Mgeta na Dakawa ambayo inachangia asilimia 34 ya mto Ruvu.

"Ilipoteza mwelekeo na sisi kama Bonde la Wami Ruvu tuliirejesha katika hali yake ya kawaida, tumechimbua mto na kuziba maeneo yote yanayopoteza maji na kusaidia kuimarisha upatikanaji maji Dar es Salaam," alisema Mmasy.

Alisema kusafisha mito hiyo kumewarahisishia Dar es Salaam kupata maji angalau ya uhakika na kwamba wameendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji na kuwaasa wananchi kuheshimu mita 60 zilizopo kisheria kwani wanachokisimamia ni kwa manufaa na mustakabali wa taifa.

Kuhusu hasara ya kurejesha mito iliyopoteza uelekeo katika hali ya kawaida, alisema ni hasara kubwa ambapo katika mwaka huu wa fedha wameshatumia zaidi ya milioni 200 kusafisha mito hivyo kuwaasa wananchi kuachana na kilimo kando ya mito na kwenye milima na miteremko mkali ili kuondoa tatizo la mito kupoteza uelekeo.

Pia, wakati wa kiangazi mamlaka za maji zimekuwa zikipata hasara kubwa kwa kutumia fedha nyingi kutibu na kusafisha maji yanayokuwa yamechafuliwa na tope kutokana na uharibifu huo unaofanyika.

Mhandisi Mmasy alisema pia mamlaka hiyo imezindua mfumo wa utabiri wa hali ya maji katika vyanzo vya maji, ili kubaini kiwango cha maji na kutoa taarifa ambapo kupitia mfumo huo wanaunganisha taarifa hizo kwa mamlaka ya hali ya hewa na kupima mtiririko wa maji ambao unaonyesha kiwango cha maji na pia kubaini kama kunaviashiria vya mafuriko.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Morogoro, Nickson Mkilanya, alisema ushirikiano uwe wa mwendelezo na kwamba wanahabari watafanya kazi kwa nia ya kuwafikisha wananchi taarifa juu ya uwepo wa Bodi ya Bonde la Wami Ruvu.

Mapema msimamizi wa kidakio cha Ruvu, Paschal Joseph, alishauri Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na wananchi kuchimba mabwawa ya kuhifadhi maji wakati huu wa mvua za masika ili yaweze kusaidia wakati wa kiangazi kwa shughuli zao.

## Mpango ataka nyumba zitakazozingatia mahitaji ya watumishi wa umma nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amesema ili kufanya Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma kuwa endelevu, ni muhimu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na halmashauri husika kuhakikisha upatikanaji maeneo ya ujenzi wa nyumba za watumishi yaliyo karibu zaidi na sehemu za kazi na yanayozingatia mahitaji ya msingi ya watumishi na familia zao kwa sasa na kwa wakati ujao.

Aliagiza hayo jana wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma unaotekelezwa na Taasisi ya Watumishi Housing Investments katika hafla iliyofanyika katika eneo la Njedengwa, mkoani Dodoma.

Alisisitiza nyumba zinazojengwa lazima zizingatie ubora na viwango stahiki ili kuendana na thamani ya fedha na kuwaepusha wanunuzi wa nyumba hizo na gharama za marekebisho na maboresho zaidi.

Makamu wa Rais alisema ili mpango huo uweze kufikia malengo yake na kuwa na manufaa kwa watumishi, ni muhimu vigezo na masharti ya upatikanaji nyumba kwa watumishi wa umma viheshimiwe na kuzingatiwa. Alisisitiza upokeaji, uchambuzi wa maombi na uthamini wa nyumba hizo vifanyike kwa haki na kuzingatia uhalisia.

Alisema juhudi za makusudi zifanyike ili watumishi wa ngazi za chini na kati wapewe kipaumbele katika upatikanaji nyumba hizo.

Dk. Mpango pia aliagiza kuzingatiwa kuwapo viwanja vya michezo, maeneo ya kupumzikia na huduma nyingine za jamii kama elimu, afya na huduma za mahitaji ya maisha, kama maduka na maeneo ya ukusanyaji taka wakati wa ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi.

Makamu wa Rais pia aliagiza watumishi na wananchi ambao watapata nafasi ya kununua nyumba hizo, kuzitunza ili zibaki katika hali ya ubora kadri inavyoyowezekana ikiwamo miundombinu na mazingira yanayozunguka eneo la nyumba. Aliwahimiza kupanda miti na maua ili kuleta mandhari nzuri na pia kuhakikisha usafi muda wote.

Makamu wa Rais alisema serikali imedhamiria kuona miradi hiyo inatekelezwa katika mikoa na wilaya zote nchini ili kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya watumishi wa umma wanaishi katika nyumba bora, na hivyo kuwawezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Alisema pamoja na kupunguza uhaba wa makazi, mradi huo pia ni kichocheo cha ukuaji uchumi kwa kutoa ajira na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya ujenzi, hususan wa makazi.



Mshtakiwa kesi ya kujipatia zaidi ya Sh.bilioni 2.74 kwa njia ya udanganyifu akidai atampatia Mitul Patel dhahabu kilo 15, raia wa Canada, Stefan Nagy (kushoto), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wanaonyanyaswa na wake zao wapewa mbinu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kimewataka wanaume kuacha kulia majumbani wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na wake zao, badala yake watoe taarifa kwenye vyombo vya kisheria, likiwamo dawati la jinsia.

Ushauri huo ulitolewa jana na Wakili kutoka TAWLA, Neema Ahmed alipozungumza na wananchi wakati wa mdahalo wa Siku ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia walioandaa kwa kushirikiana na Ushirika wa Wakulima wa Zabibu na masoko Mpunguzi, kata ya Matumbulu, jiji la Dodoma.

Ahmed alisema bado kuna wanaume wanafanyiwa vitendo vya kikatili, lakini wanaishia kulia ndani ya nyumba zao, hivyo chama hicho kinawataka watoe taarifa hizo ili wapatiwe msaada wa kisheria.

Alisema vitendo vya kikatili si tu vile vilivyozoeleka, hata kupigwa na kunyimwa unyumba ni ukatili, hivyo wanapofanyiwa na kukaa kimya kwa kisingizio cha kuona aibu, wanakosa haki ya msingi ya kupatiwa utetezi.

"TAWLA inawaomba kinababa mnaofanyiwa vitendo hivyo vya kikatili na wake zenu, nendeni kwenye vyombo vya kisheria ili mtetewe na kupata haki zenu za msingi badala ya kuendelea kulia humo majumbani mwenu," alisema.

Polisi Kata ya Matumbulu Dawati la Jinsia, Gwantwa Kabuye, alizitaka familia kuacha tabia ya kumalizana kesi zinazohusiana na ubakaji pale inapotokea, badala yake wajenge mazoea ya kwenda kwenye vyombo vya kisheria ili haki itendeke.

Kabuye alisema bado kuna familia mtoto amebakwa au kulawitiwa, zinamalizana bila kutambua kuwa waliofanyiwa wanaathirika na kupata maumivu makali kwenye maisha yao yote.

"Unakuta mjomba amefanya kitendo hicho cha ubakaji au kulawiti, badala ya kutoa taarifa kwenye vyombo vya kisheria wanakaa kama wanafamilia na kumalizana bila kutambua kuwa hatua hiyo ni makosa ya jinai na yanatakiwa kupelekwa polisi na mahakamani," alisema.

Diwani wa Matumbulu, Emmanuel Chibago alizitaka familia kusomesha watoto wao badala ya kuwaozesha, kuchunga mifugo na kuwatafutia kazi za ndani kwa kuwa hivyo ni vitendo vya kikatili vinavyomkosesha mtoto haki ya kupata elimu.

Alisema baadhi ya familia zina watoto ambao wamekuwa wakiwafanyia vitendo vya kuwanyima haki za kimsingi kwa kuwaozesha, kuchunga mifugo na kuwatafutia kazi za ndani badala ya kuwasomesha ili waondokane na umasikini.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA ARUSHA, KILIMANJARO NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA CHEMBA, KONDOA NA MJI WA KONDOA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dodoma katika Halmashauri za Wilaya za Chemba, Kondoa, na Mji wa Kondoa kuanzia tarehe 11 hadi 17 Desemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 11 hadi Jumanne tarehe 17 Desemba, 2024.
2. VITUO: Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua namba 3 (Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 03 Desemba, 2024 na:

**Livini A. Morrice**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218284201

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Matumizi nishati safi yapunguza uharibifu mazingira*

**MIAKA** ya nyuma kabla ya kampeni ya matumizi ya nishati safi haijapamba moto, usafirishaji mkaa kutoka mikoani ulishamiri na uharibifu wa mazingira ulikuwa katika hali mbaya.

Kwa mifano michache kwa wanaopita Barabara ya Bagamoyo, ilikuwa huwezi kutembea bila kukutana na pikipiki au malori yaliyosheheni magunia ya mkaa.

Ukiangalia idadi ya magunia yaliyopakiwa kwenye malori hayo, utagundua ni jinsi gani misitu ilivyokuwa ikiangamia kwa kukatwa miti inayochomwa na kuwa mkaa.

Mbali na uharibifu wa mazingira, lakini matumizi ya kuni na mkaa yana athari kubwa katika afya za binadamu kutokana na moshi wanaouvuta.

Matumizi ya nishati safi ya gesi imesaidia kwa kiasi kikubwa kuepuka uchafuzi wa hewa ambao unasababisha uharibifu wa mazingira na pia kusababisha magonjwa mbalimbali.

Ulinzi wa afya ya mama, familia, mazingira na taifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima uanzie jikoni.

Mkutano Mkuu wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (TOA), ulieleza kuhusu tamanio la serikali kufikia asilimia 80 ya Watanzania wote kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara wa kutangaza matumizi ya nishati safi ya kupikia na lazima taifa lianze sasa kubadilisha nishati inayotumiwa kupikia.

Mara kwa mara anapokuwa kwenye majukwaa mbalimbali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Rais anasema huwezi kumaliza au kupunguza ukataji miti unaoangamiza misitu kama hutaligusa jiko.

Kampeni ya Rais imefanya mengi, Watanzania wameelezwa umuhimu wa matumizi ya teknolojia za kupikia zinazopunguza madhara kiafya, athari kwa mazingira na kijamii.

Na sasa Rais amelifikisha taifa kwenye kutekeleza Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034.

Analenga kaya zenye 'jiko safi na salama', ambayo asilimia 80 ya Watanzania watakuwa wanatumia jiko lenye nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Pamoja na kuwaondoa kinamama katika matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi, pia taasisi kubwa ambazo zinahudumia watu wengi kupata chakula, zinahimizwa kuhama kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ili kupunguza uharibifu wa hewa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, ili kufanikiwa katika matumizi ya nishati safi ipo haja ya kuwa uhamasishaji wa kutumia majiko yanayotumia nishati safi na yapatikane kwa urahisi ili wanayoyahitaji wasipate vikwazo kwa kuyapata.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) inaeleza kuwa Tanzania Bara ina takribani kaya milioni 13.9.

Kufikia azma hiyo kaya zenye jiko safi na wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie matumizi ya nishati safi ya kupikia na pia wizara na taasisi za umma kadhalika na sekta binafsi kuzingatia matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira na kuepusha athari nyingi zinazotokana na kutumia nishati zisizo safi.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliagiza taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, ifikapo Januari, mwaka huu, ziache kutumia kuni na mkaa kupikia.

Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mikakati yake inaeleza kuwa hilo limefanyika na taasisi nyingi zikiwamo za umma kuanzia Magereza, kambi za jeshi, shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vikuu vimeanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Pia, juhudi zinafanywa na kila taasisi inayohusika na nishati na katika mbio za Mwenge wa Uhuru, mwaka huu, ujumbe mkubwa unaobebwa ni uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi kupikia.

Uhamasishaji huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuepusha athari zinazosababishwa na hewa chafu inayotokana na kuvuta moshi mchafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Tuntule Swebe

### Muungwana Lazima Nilonge

## *Tuache kunadi watoto wetu kuwa ombaomba, tujali kesho yao yaja*

**SOTE** tunafahamu jamii inayotuzunguka, ina watu tofauti, kwani kuna wenye kipato na wasio nacho, kuna walemavu na wasio nacho.

Jambo la kushangaza kuna baadhi ya watu kwenye jamii yetu wanawatumia watoto hao kuwapa faida, pasipo kuzingatia utu katika hilo.

Wanawahangaisha watoto hao juani, wakiomba pesa zinazotumika kwa maslahi yao. La kushangaza, hata wakati wa mvua, watoto hao huwekwa barabarani.

Walichokisahau ni kwamba, watoto wengine wana fursa, pale wanapowezesha, kwani kuna baadhi yao watoto wamejiunga kwenye vyuo vya ufundi na wamekua na uwezo wa kujitegemea.

Lakini kuna wazazi hawaelewi, wanawatenga watoto, pasipo kujua wa wanawaumiza, kiasi gani wanawaharibu, kimazingira na hata kutoka kwa maadui wengine.

Kuna wengine wanawavusha watoto hao kwenye mipaka kuwatumia katika shughuli za kipato, jambo linaloashiria utumwa kwa wanaofanyiwa hayo, hata vyombo vya kimataifa tunaona vinaripoti hayo kinachojiri huko ughaibuni.

'Tumeshachukua hatua kuhusu kutumiwa kwa watoto kuwa 'ombaomba'...", serikali nchini ilishawahi kukiri kuwapo baadhi ya watu wanaofanya biashara haramu ya ulanguzi wa binadamu.

Hilo linafanyika kwa kuwasafirisha watoto wenye ulemavu na kisha kuwatumikisha kwenye shughuli mbalimbali, zikiwamo za 'ombaomba'.

Hata hivyo, inaelezwa serikali inaendelea na juhudi za kutoa elimu, kuwatambua walemavu na kuongeza ulinzi mipakani, ili kuhakikisha biashara hiyo inakomeshwa.

Kiserikali ilishatamka kwamba, kama sehemu ya jamii inatakiwa kuwa kioo kwa wengine, baadhi ya watu kwenye nchi wamekuwa hodari kuwasaidia walemavu na kuwapa furaha.

Mfano, aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni ya IPP Media, Hayati Reginald Mengi, akaweza kuwapa ajira baadhi ya wenye ulemavu wenamudu kufanya kazi, bayana kwa mustakabali mpana akazidisha upendo kwa watu kada hiyo.

Ameweza kuwafanyia sherehe kila mwaka na kujumuika nao kwa chakula maalum cha jioni, akionyesha thamani na umuhimu wa jamii hiyo.

Inajulikana kwamba, kila binadamu katika maisha yake yanayoendelea, hakuna anayejua hatima ya kesho yake.

Hali ya kuwa na viungo vilivyokamilika sasa, ni jambo la kumshukuru na kuwasaidia wasiokuwa nacho au wasiojiweza, nao ni wajibu wa kibinadamu.

Inatupasa kukumbuka kuwa, maisha yanazungukwa na ajali zinazoweza kusababisha kupoteza viungo, ambavyo ni nguzo zetu muhimu.

Pia, kuna magonjwa yanayotuachia ulemavu, hivyo tusimame na dhana "usilopenda kutendewa, usimtendee mwingine."

Nilisoma, katika habari ni moja ya kimataifa miezi kadhaa iliyopita ni kwamba, baadhi ya walemavu wanapata changamoto.

Katika ulimwenguu huo ambao mara nyingi huhusisha mafanikio na ukamilifu wa kimwili na kiakili, ni muhimu kufahamu kuna watu wenye ulemavu wamevuka magumu na kutenda mambo makubwa, yanayoweza kugeuka mifano inayoweza kuwa ya kuigwa duniani.

Katika historia, kuna watu wengi maarufu wenye ulemavu, sio tu kwamba wamebadili mitazamo na matarajio ya jamii kwamba hawana uwezo, pia wameacha alama isiyofutika katika nyanja zao husika.

Ni vizuri tukaendelea kujumuika wote kusimama pamoja, katika falsafa hii ya kuwatambua wenye ulemavu na wakatetea haki zao.

Naamini vyote vinawezekana, maana hata mfano ni mifumo mingi inayohusu ujenzi sasa nchini ni rafiki na maisha ya wenye ulemavu.

Tunaweza kuvuta hisia mbali, hata harakati za haki za kijinsia zilichukua sura hizo na zilikofika imekuwa falsafa ya umma, huku vita kuziba mapengo mbalimbali ya haki hizo inaendelea.

Hicho ndicho ninaamini kwa wenye ulemavu, tuwapiganie kwa kasi na falsafa ya mkuu wa nchi yetu 'Kazi Iendelee.'

HABARI KITAIFA

# IAA kutumia teknolojia kufundisha madarasa janja

**Na Grace Mwakalinga,** ARUSHA

KATIKA kuboresha utoaji huduma na kuwafikia wanafunzi wengi zaidi, Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kimepanga kutumia teknolojia ya kisasa ya madarasa janja, kufundisha mwanachuo au mhadhiri kuwapo darasani.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati wa ziara ya wahariri wa vyombo vya habari nchini, Mkuu wa IAA, Prof. Eliamani Sedoyeka alisema kwa kuanzia chuo kimenunua mifumo 35 ya kuwezesha utolewaji mafunzo hayo wanayoyaita "smart classes".

Alisema kwa sasa kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), chuo kimepokea dola za Marekani milioni 21 sawa na zaidi ya Sh. bilioni 56 ambazo ni mkopo wa riba nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB).

"Katika mradi huu wa HEET, tunajenga madarasa 'smart', ambayo yatakuwa na miundombinu inayotumia teknolojia za kisasa, mifumo hiyo itasaidia kuwatambua wanafunzi na kufahamu maendeleo yao ya elimu," alisema Prof. Sedoyeka.

Akifafanua zaidi, Prof. Sedoyeka alisema matumizi ya mifumo hiyo ya kufundishia yatawezesha utolewaji elimu bora kulingana na mahitaji ya wanachuo.

"Awali tulikuwa tunatumia rasilimali nyingi kuhakikisha wanachuo zaidi ya 16,000 wanasoma, lakini sasa mwanafunzi au mhadhiri hatowajibika tena kuja chuoni, michakato yote ya ufundishaji ikiwamo maudhui au kuuliza maswali, vinaweza kufanyika kwa njia ya mtandao," alisema Prof. Sedoyeka.

Alisema kuwa mbali na kuboresha mifumo ya utoaji elimu, pia watajenga madarasa janja ambayo yataunganishwa na teknolojia za kisasa zitakazotumika katika ufundishaji na kufuatilia maendeleo ya mwanachuo.

Msanifu Majengo wa Mradi wa Jengo la Utawala IAA, Monica Emmanuel, alisema mradi huo umefikia asilimia 90, wakitumia Sh. bilioni 10 kati ya Sh. bilioni 13 zilizotengwa na unatarajiwa kukamilika Machi mwakani.

"Jengo hili likikamilika, litakuwa na eneo la utawala, madarasa, sehemu ya kutolea huduma za afya na studio ya kisasa kwa ajili ya kutoa maudhui ya habari," alisema Monica.

**Jengo hili likikamilika, litakuwa na eneo la utawala, madarasa, sehemu ya kutolea huduma za afya na studio ya kisasa kwa ajili ya kutoa maudhui ya habari.**



Mwenyekiti wa Bodi ya Tuzo za Taifa za Uandishi Bunifu za Mwalimu Nyerere, Prof. Penina Mlama, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akiwasisitiza Watanzania kujitokeza kwa wingi kuwasilisha miswada katika kipengele cha tamthilia ili kushindania tuzo hiyo. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Upinzani wataka nguvu ya pamoja kudai Katiba mpya

**Na Jenifer Gilla**

VYAMA vya upinzani nchini vimesema kunahitajika nguvu ya pamoja ya wadau wa siasa kupigania Katiba mpya na maboresho katika mifumo ya uchaguzi ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki na kuepuka yaliyotokea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Ni rai iliyotolewa juzi wakati wa mdahalo ulioandaliwa na Mtandao wa Jamii Forums kwa ajili ya tathmini ya Uchaguzi wa Serikali ya Mitaa, ukiangazia ukiukwaji wa sheria za uchaguzi na mambo ya kujifunza.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA), John Pambalu alisema ili kurekebisha yaliyotokea katika uchaguzi huo, viongozi wa vyama vya upinzani, wanazuoni, viongozi wa dini, watu mashuhuri na makundi mbalimbali wanapaswa kuungana na kupigania mabadiliko ya Katiba yatakayoleta uchaguzi huru na wa haki.

Alisema nchi inapojiandaa kwa Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Novemba mwakani kunahitajika nguvu ya umma kuibana serikali, ili kuwapo Katiba mpya au kufanya maboresho madogo katika mifumo ya uchaguzi, hivyo kushughulikia mambo yote yanayohusiana na uchaguzi kikatiba na si kikanuni.

"Ninachokiona mimi ni muda mwafaka kuwa na mazungumzo na wadau wote wa demokrasia, haki za binadamu na utawala bora ili kwa pamoja tushinikize watawala (serikali) tushirikiane kuandika Katiba mpya ama kufanya marekebisho madogo," alishauri.

Alisema uchaguzi huo uliambatana na matukio mengi ambayo yaliashiria kukiukwa sheria za uchaguzi, ikiwamo kuandikisha watoto na marehemu kwenye daftari la wakazi, vyombo vya ulinzi na usalama kuhujumu uchaguzi kwa kuweka kura katika maboksi ya kura na hata kufanya mauaji.

Pambalu alisema matukio hayo yanapaswa kutumika kama funzo la kuona haja ya kufanya maboresho katika mifumo ya uchaguzi.

"Kwa hiyo, sisi kama chama (CHADEMA) tunatoa wito sasa, ni wakati sahihi kwetu wadau kuunganisha nguvu za pamoja kupigania Katiba itakayoleta haki na usawa katika masuala ya uchaguzi," alisema.

Pambalu alisema mabadiliko yoyote duniani hayakutokea kwa njia rahisi, bali kuna makundi ya watu yalijitoa mhanga ili kuleta mabadiliko hayo.

Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Vijana wa Chama cha Wananchi (CUF), Iddi Mkanza, alitoa wito kwa mashirika kimataifa ya kidemokrasia kuingilia kati na kuwaunga mkono katika kuboresha demokrasia nchini.

Mkanza alisema kuwa ikiwezekana washirika wa maendeleo wasitishe misaada wanayotoa kwa Tanzania, akidai kuwa hivi sasa inanufaisha chama kimoja.

Alisema kuwa licha ya matokeo ya uchaguzi huo kuonesha Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeshinda kwa asilimia 99, kuna vijiji vingi ambavyo wagombea kutoka vyama vya upinzani walienguliwa na maeneo mengine wapigakura waliingia na kukuta wagombea ni wa chama kimoja.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha ACT - Wazalendo, Ester Thomas, alidai wananchi wanapaswa kutambua kuwa waliohujumu matokeo ya uchaguzi huo ni watumishi wa umma, likiwamo Jeshi la Polisi, walimu na watendaji wa vijiji na TAMISEMI ambayo ndiye msimamizi mkuu.

Alisema vyama vya siasa vilikuwa tayari kufanya marekebisho ya mifumo ya uchaguzi na ndio maana walijiunga katika kikosi kazi cha utekelezaji wake, lakini anahofu kama mapendekezo waliyotoa yanafanyiwa kazi au la.

Katibu Mkuu wa Chama cha Sauti ya Umma (CHAUMA), Majalio Kyara, alipongeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikisha vyama vya upinzani tangu mwanzo wa uchaguzi ingawa utekelezaji wa waliyokubaliana una mambo ambayo yaliwabana wakati wa uchaguzi huo.

KABWELA **Na Fadhil Mohammed**





Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), akimpa zawadi ya bidhaa mbalimbali za chai inayozalishwa nchini, Mkurugenzi wa Miradi ya Maendeleo Kampuni ya Kawasaki Kiko ya Japan, Hirofumi Suganuma, jijini Dodoma juzi, alipokutana naye pamoja na ujumbe wake wa watu watano waliokuja nchini kuangalia fursa na kubadilishana uzoefu katika zao la chai. Katikati ni Ofisa Ubalozi anayeratibu Masuala ya Uchumi Ubalozi wa Tanzania nchini Japan, Edna Chuku. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Mwigulu atoa onyo watoa huduma fedha

**Farida Ramadhani na Chedaiwe Msuya**

SERIKALI imesema itaendelea kuchukua hatua kali kwa taasisi zote zinazotoa huduma za fedha kinyume cha sheria kwa kutoa mikopo umiza (kausha damu) na kuwakandamiza wananchi.

Onyo hilo limetolewa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati akizindua Jukwaa la kwanza la Wadau wa Sekta ya Fedha kwa mwaka 2024.

Alisema taasisi hizo zinawaumiza wananchi kwa kutoa mikopo yenye riba kubwa pamoja na kupanga njama za kuwafilisi wakijua hawatoweza kulipa.

Aidha, aliwataka wadau wa sekta ya fedha hususan benki kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kutumia huduma rasmi za fedha kwa kutumia taasisi ambazo zimesajiliwa, ili kuepukana na madhara wanayokumbana nayo katika taasisi nyonyaji zinazotoa mikopo umiza.

Alisema vyema wadau wa sekta ya fedha wawaelimishe wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia benki kupata mikopo pamoja na kutunza fedha benki ni utaratibu wa kisasa wa uendeshaji wa uchumi.

"Bado kuna baadhi ya maeneo wananchi wanaogopa kuweka fedha benki, kwa kuwa nyinyi mpo kwenye sekta hii mshirikiane na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwaeleza wananchi kuwa wasiogope kuweka fedha benki," alisema.

Alisema pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kukusanya kodi kwa weledi na kwa kufuata sheria wananchi hawajaeleweshwa vizuri kuhusu kuweka fedha benki.

Aliwaagiza viongozi wa taasisi za fedha nchini kujiridhisha kabla ya kuruhusu watumishi na madalali wao kupiga minada ya mali za wadaiwa mikopo kwenye taasisi zao kutokana na taarifa kuwa baadhi ya watumishi wasio waaminifu hushirikiana na watu wengine kuwadhulumu mali zilizowekwa kama dhamana na kuwatia watu umasikini.

"Kuna baadhi ya maeneo hakufanyiki vizuri katika kudai mikopo, mteja amelipa mkopo wake kwa asilimia 80, amebakiza asilimia 20, anatokea mteja mwingine anapenda dhamana ya mkopo iliyowekwa, benki inaamua kupiga mnada.

"Muda mfupi ambao wanajua mteja hatoweza kulipa ili wamfilisi, mtu amelipa mkopo kwa asilimia 80 halafu unauza dhamana yake ili kufidia asilimia, sio utaratibu mzuri wa kujenga ustawi wa jamii," alisema Dk. Nchemba.

Aliziagiza benki kuwachukulia hatua baadhi ya watumishi wa benki wasio waaminifu ambao wanashirikiana na baadhi ya wateja kuongeza mikopo chechefu.

Aidha, alisema kutokana na kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo ndio maana Tanzania ni miongoni mwa nchi mbili pekee barani Afrika zenye uhimilivu wa deni na kwa Afrika Mashariki na nchi zilizopo katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Tanzania inaongoza.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema mwakani serikali itaanzisha mtaala mpya wa masomo ya masuala ya fedha na ujasiriamali ambayo yatakuwa ni lazima ili wanafunzi watakapomaliza wajiajiri.

Aliwataka wadau mbalimbali kuendelea kutoa maoni kuhusu mtaala huo ili kuuwezesha kufikia lengo kusudiwa.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu El-maamry Mwamba, alisema Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Fedha nchini imeandaa Jukwaa la wadau wa Sekta ya Fedha ili kubadilishana mawazo na uzoefu, kupeana taarifa, kujengeana uwezo, kushirikishana katika mafanikio na changamoto na kutafuta suluhu ya pamoja kwa changamoto zinazoikabili sekta ya fedha nchini.

Alisema malengo ya jukwaa hilo ni pamoja na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kwa kipindi cha miaka mitatu (2020/21-2023/24) na kushirikishana mbinu bora za kiutendaji na uzoefu katika Sekta ya Fedha.

Dk. Mwamba alisema malengo mengine ni kujadili fursa na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kuboresha sekta ya fedha pamoja na kushirikishana namna bora ya kukuza matumizi ya teknolojia na uvumbuzi ili kukuza na kuimarisha sekta ya fedha.

Jukwaa hilo pia linalenga kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wadau wa sekta ya fedha na kuufahamisha umma hatua za maboresho mbalimbali ya kisera na kisheria yaliyofanyika ili kuimarisha sekta ya fedha nchini.

# Mtanzania ashinda tuzo ubunifu udhibiti wadudu mazao 2024

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MWANASAYANSI wa kike Mtanzania, Dk. Never Mwambela, ameshinda tuzo ya juu ya ubunifu Agro ecological Food Futures Prize 2024 katika ukanda wa Afrika Mashariki, akiwaacha nyuma washindani zaidi ya 200.

Dk. Mwambela ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo cha Afrika cha Wanyamapori Mweka, alitunukiwa tuzo hiyo katika hafla iliyofanyika hivi karibuni jijini Kigali, Rwanda.

Mshindi huyo ni Mwanzilishi na ni Afisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Plant Biodefenders, ya mjini Moshi inayotengeneza dawa ya viwatilifu ya vuruga, suluhisho rafiki wa mazingira la kudhibiti wadudu hatari katika kilimo, huku ikichangia maendeleo endelevu ya kilimo licha ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Mwambela alieleza changamoto zinazokumba kampuni yake, hususan katika kupata fedha za kupanua uzalishaji na za kumuwezesha kuwafikia wakulima wengi zaidi.

"Bidhaa zetu ni uvumbuzi wetu ni muhimu, lakini kuwafikia watu bado ni changamoto kubwa. Tuzo hii itawawezesha mafunzo kwa wakulima 10,000 ili kuongeza ufahamu kuhusu bidhaa zao endelevu," alisema.

Alieleza maono yake ya kupanua suluhisho lao kwa nchi nyingine za Afrika zinazojiandaa kukabiliana na changamoto za wadudu, akisisitiza haja ya kupunguza utegemezi kwa dawa za kilimo za kemikali.

Aidha, alihimiza ushirikiano na uwekezaji ili kushinda changamoto za kifedha na kufikia masoko mapana.

Katika mkutano wa kimataifa uliojaa wataalamu wa kilimo na uhifadhi wa mazingira, Dk. Mwambela alisema, "Tunawaokoa wanadamu na viumbe hai kwa ugunduzi bora."

Alisema changamoto kubwa inayoikumba sekta ya kilimo ni pamoja na hasara ya mazao kati ya asilimia 20-40 kutokana na uharibifu wa wadudu.

Alitaja takwimu kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Mwambela alisema gharama ya kudhibiti wadudu duniani inakadiriwa kufikia dola bilioni 220, kudhibiti wadudu waharibifu pekee zinatumika dola bilioni 70 kila mwaka.

Alisema wadudu kama mende wa shamba la mahindi (fall armyworm), mdudu kama Kanitangaze (Tuta absoluta) inayoshambulia nyanya, na borer wa kahawa (coffee berry borer) wanavyoharibu mazao muhimu, huku akionesha dawa za kilimo za kemikali zina gharama kubwa na zina athari kubwa za kiikolojia.

Alisisitiza kuwa dunia inahitaji suluhisho la uvumbuzi, linaloweza kudumu na linalohakikisha usalama kwa mazingira na afya.

Aidha, alisema Dawa ya Vuruga ni kiwatilifu cha kipekee kinachotokana na fangasi, isiyo na sumu na ambayo haiwezi kusababisha usugu kutoka kwa wadudu waharibifu wa mazao.

"Inapoongeza mavuno na kuhamasisha wadudu vuvuzaji, Dawa ya Vuruga ni suluhisho linaloongeza usalama wa chakula," alisema.

Dk. Mwambela alielezea faida nyingine za Dawa ya Vuruga, ikiwa ni pamoja na kuimarisha afya ya udongo, kupunguza matumizi ya dawa za kemikali, na kuvutia wadudu asili wanaoshambulia wadudu waharibifu.

Vilevile, alieleza kuwa Dawa ya Vuruga ina uwezo wa kukaa bila kuharibika kwa miezi 12, na imethibitishwa na Bio Inspector kama suluhisho bora la kuua wadudu kwa ufanisi wa asilimia 90-100.

Dk. Mwambela alifafanua athari nzuri za kampuni yake, Plant Biodefenders, ambayo imesaidia wakulima 11,500, ikiwa na sajili nne na bidhaa sita, na kwamba kampuni imefanikiwa kuokoa ekari 300,000 za mazao, kuokoa tani 160,000 za pamba, na kulinda mazao muhimu kama kahawa.

Alisema kuwa licha ya mafanikio hayo, bado wanahitaji uwekezaji wa dola 500,000 kupanua biashara yao, kutengeneza mbolea za kibaiolojia, na kufikia masoko mapya.

Balozi wa Tanzania nchini Rwanda, Abdalla Nangwanda, alielezea furaha yake kwa kumpongeza Dk. Mwambela kwa mafanikio yake makubwa, akisema kuwa mafanikio haya yanainua taifa zima na vijana wengine kufuata nyayo.

Tuzo ya Agroecological Food Futures, iliyoanzishwa na Biovision Foundation, IKEA Foundation, na Shirika la Usimamizi wa Maendeleo la Uswisi (SDC), inalenga kusaidia biashara ndogo na za kati zinazozingatia misingi ya kilimo cha kiikolojia.



## Watoto wa kike watajwa ukatili kwa baba zao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWENYEKITI wa Kijiji cha Lole Kata ya Mwika Kaskazini wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro, John Safiel amesema aina mpya ya ukatili unaoitesa jamii katika eneo hilo ni wanaume kwenye ndoa kuandaliwa hadi maji ya kuoga bafuni na watoto wao wa kike.

Akizungumza jana wakati wa mdahalo wa kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kama sehemu ya Maadhimisho ya Siku 16 kupinga ukatili duniani, Safiel, alieleza namna kundi hilo la wanawake walioko kwenye ndoa, linavyoweka kando jukumu lao la kuwatwisha watoto wao, hasa wa kike.

"Hapa kwetu Mwika baadhi ya wanawake wamesahau wajibu wao kwa waume zao kama vile kuwapikia, kuwapashia maji na kuwapelekea bafuni; badala yake wanawatwisha watoto wao kazi, ambazo walitakiwa wazifanye. Sasa jambo hili linachangia kuchochea ukatili dhidi ya watoto," alisema.

Safieli, alisema serikali ya kijiji hicho inaendelea kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la KWIECO kupinga vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto na kuwataka wanaume kusimama katika nafasi zao kwa kuwajibika kuhudumia familia.

Alisema anawaunga mkono wanawake kwa kuwa wamekuwa wakishiriki katika maendeleo ya kijiji hicho, huku akieleza namna KWIECO lilivyogeuka chachu ya mabadiliko katika haki za wanawake, watoto na uchumi.

Mmoja wa wanawake wa kijiji hicho, Salome Shao, alisema kumekuwepo na mabadiliko makubwa katika jamii ya Kichaga kwa sasa kwa mwanamke kushiriki katika fursa za uchumi na kutoa maamuzi katika ujenzi na shughuli nyinginezo za maendeleo.

Exaud Shao, alisema kutokana na wanawake kuwa na uchumi mkubwa, kumesababisha ndoa nyingi kuvunjika na watoto kuishi katika mazingira hatarishi kwa kukosa malezi ya wazazi.

Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na KWIECO kwa ufadhili wa na Women Fund Tanzania Trust (WFT), Veronica Ollomi, alisema mengi ya mambo ambayo yanatikisa kwa sasa katika jamii ya Kilimanjaro ni makosa ya ukatili wa kingono.

**Hapa kwetu Mwika baadhi ya wanawake wamesahau wajibu wao kwa waume zao kama vile kuwapikia, kuwapashia maji na kuwapelekea bafuni; badala yake wanawatwisha watoto wao kazi walizotakiwa wazifanye.**

# 'Serikali iongeze likizo ya uzazi kwa wanawake'

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWANAHARAKATI Aginatha Rutazaa, ameiomba serikali kufikiria upya ombi la wafanyakazi nchini la kuongezewa likizo ya uzazi kutoka siku 84 hadi miezi sita, ili wanawake kupata muda zaidi wa kuwahudumia watoto wanaozaliwa.

Akizungumza katika Mji wa Moshi, wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Siku 16 za kupinga ukatili, alisema kuongezwa kwa likizo hiyo kutasaidia kupunguza ukatili dhidi ya watoto unaofanywa na wasichana wa kazi majumbani, kipindi ambacho ni cha ukuaji wa mtoto.

"Kwa sababu baada ya siku 84, ndio mtoto anaanza kukaza shingo na hapo anaachiwa msichana wa kazi, ambaye hujui ametokea wapi na saa nyingine hana maadili yale unayoyategemea.

"Watoto wengi wa umri huo, ndio wanaofanyiwa ukatili kwa sababu unakuta wazazi wanakimbizana na kazi za ofisini ili wasifukuzwe kwenye vibarua vyao."

Aliongeza: "Tumeona matukio ya ukatili wa kingono yanatokea sana hasa katika ngazi za familia, na hii inatokana na wale wamama, wadada wanaopata watoto katika umri ambao bado, hawana nguvu za kufanya kazi za kiuchumi.

...Tunaomba serikali ifumue sheria hiyo na iongeze muda ili waweze kukaa nyumbani, hata kwa miezi sita badala ya siku 84, ili mtoto yule aweze kukomaa. Katika nchi zilizoendelea wamama wanakaa nyumbani hata mwaka mzima."

Mwezi Mei mwaka huu, serikali ilikubali kuongeza muda wa likizo peke yake ya uzazi kwa wanaojifungua watoto njiti.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alinukuliwa akisema likizo ya uzazi ni miongoni mwa haki za wafanyakazi ambazo hutolewa kwa muda wa siku 84, endapo mfanyakazi atajifungua mtoto mmoja au siku 100 zaidi ya mmoja.

Alisema mfanyakazi huyo ataruhusiwa kutoka kazini saa saba mchana kila siku kwa miezi sita baada ya kumalizika kwa likizo ya uzazi ili kumpa ruhusa ya kwenda kunyonyesha.

**Watoto wengi wa umri huo, ndio wanaofanyiwa ukatili kwa sababu unakuta wazazi wanakimbizana na kazi za ofisini ili wasifukuzwe kwenye vibarua vyao.**



Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, James Ole Millya (kushoto), akiwavalisha mavazi ya jadi wawekezaji raia wa China, walipotembelea migodi ya madini ya Tanzanite, katika mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Serikali yafichua migogoro ya ndoa K'njaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JUKWAA la wanaharakati wa kupambana na ukatili wa kijinsia mkoani Kilimanjaro limesena migogoro mingi ya ndoa inasababishwa na baadhi ya wanawake kukosa heshima kwa waume zao baada ya vipato vyao kuimarika.

Msemaji wa mashirika 12 ya kiraia yaliyotoa tamko jana la kulaani ukatili huo, Wakili mkongwe nchini na mwanaharakati wa haki za binadamu, Elizabeth Minde, alisema kundi rika la miaka 30 hadi 45 ya wanawake, wameonekana kulalamikiwa maeneo mbalimbali.

"Wengine wakisema 'hawa wapora wadogo (mke mdogo) wanawaonea sana waume zao' mfano halisi ni nukuu kutoka katika mjadala wa kijamii uliofanyika Kata ya Mwika Kaskazini.

"Sisi wanaharakati tunasema kuwa kuimarika kwa kipato cha mwanamke kisiwe chanzo cha migogoro ya ndoa. Muhimu ni kuimarisha mawasiliano, mahusiano na maamuzi shirikishi katika bajeti za familia, matumizi ya muda kwa uwazi na uwajibikaji wenye ustawi chanya na ulioendelevu ndani ya familia."

Wanaharakati hao wameeleza kiini cha migogoro hiyo pia kinachagizwa zaidi na kuimarika kwa fursa za kiuchumi kwa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa Wakili Minde, wanawake wengi wa mkoa huo kwa sasa ni wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wengi wao ndio wenye mitaji katika masoko makubwa kama Soko la Kumbukumbu ya King George (Meimoria) na kwa Sadala.

Alisema wanawake katika wilaya za Rombo na Halmashauri ya Moshi ni mifano ya wanunuzi na wauzaji wakubwa wa mazao ya ndizi, parachichi na bidhaa nyingine za maduka ya nguo, ikilinganishwa na miaka ya 1995.





Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Nyabaengere, Kata ya Musanja Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiwa nje ya zahanati mpya ya kijiji hicho iliyofunguliwa juzi na kuwapunguzia wanakijiji adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ukatili, udhalilishaji nchini bado pasua kichwa

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limesema bado linakabiliwa na tatizo la kukosa ushahidi kwa kesi za ukatili na udhalilishaji kijinsia kutokana na wahusika kumaliza kifamilia nyumbani.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Wilbroad Mutafungwa (pichani) katika kilele cha Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili na Siku ya Haki za Binadamu yaliyofanyika juzi jijini hapa.

Kwa mujibu wa Mutafungwa, licha ya tatizo hilo, matukio ya ukatili yaliyoripotiwa mwaka 2023 yamepungua kwa zaidi ya 20 kwa mwaka 2024 sawa na zaidi ya asilimia 1.9. Alisema wamefanikiwa kupunguza matukio hayo kutoka 1,140 mwaka 2023 hadi 1,118 mwaka huu sawa na upungufu wa matukio 22.

Alisema kupungua kwa matukio hayo, kumetokana na jitihada zinazofanywa na jeshi hilo kupitia Mtandao wa Polisi Wanawake (TPF NET), Dawati la Jinsia na Watoto na Polisi Kata kutoa elimu na kuchukua hatua dhidi ya watuhumiwa.

Mutafungwa, alisema tatizo lililopo ni kesi nyingi za ukatili kukwama kwa

**Kufanya hivyo tunakuwa tunaendelea kuulea ukatili na tunakuwa hatujatimiza wajibu. Polisi tunaendelea kutoa elimu kuhakikisha jamii inatambua makosa haya ya unyanyasaji wa kijinsia na watoto na kuyatolea taarifa.**



kukosa ushahidi kutokana na wahusika kumalizana nyumbani.

"Kufanya hivyo tunakuwa tunaendelea kuulea ukatili na tunakuwa hatujatimiza wajibu. Polisi tunaendelea kutoa elimu kuhakikisha jamii inatambua makosa haya ya unyanyasaji wa kijinsia na watoto na kuyatolea taarifa," alisema.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi aliitaka jamii kupinga ukatili wa kijinsia na watoto nchini.

Makilagi, aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vinavyohusika na mapambano dhidi ya vitendo hivyo ili kuhakikisha vinatokomezwa katika jamii.

Baadhi ya wadau wa maendeleo ya jamii walioshiriki maadhimisho hayo, walitaja chanzo cha kukithiri kwa ukatili nchini ni pamoja na tatizo la afya akili.

Waliliomba jeshi hilo kuendelea kushirikiana na wadau kukemea na kuwachukulia hatua watuhumiwa ili iwe fundisho kwa wengine.

**KISHAPU NAO WANENA**

Wakati huo huo; baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga wamedai jamii ya maeneo ya vijijini wanafumbia macho vitendo vya ukatili kwa kumaliza kesi hizo kifamilia kutoka na waogo na kujiepusha na uhasama miongoni mwao.

Wakazi hao, akiwemo Shida Masalu, walitoa madai hayo kwenye maadhimisho hayo ambayo kwa Mkoa wa Shinyanga yalifanyika Kata ya Shagihilu wilayani humo.

Masatu, alidai siyo kwamba matukio hawayaoni na hawajuhi mahali pa kutoa taarifa, wamekuwa wakiogopa uhasama na kwenda kutoa ushahidi mahakamani.

Alisisitiza elimu iendelee kutolewa zaidi kwa kazi hao ya kuwajengea ujasiri wa kutoa taarifa za matukio hayo na ushahidi mahakamani dhidi ya watuhumiwa.

Kwa mujibu wa Utafiti wa Maendeleo ya Watu na Afya Tanzania (TDHS), mwaka 2010 matukio ya ukatili wa kijinsia mkoani Shinyanga yalikuwa asilimia 34 na kwa mwaka 2022 yalipungua na kufikia asilimia 28.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringa Macha katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, aliwataka wananchi kutoa taarifa za matukio ya ukatili hayo kwenye vyombo husika, ili hatua zichukuliwe.

Mkude, alisema kuyafumbia macho matukio hayo ni kuifanya jamii kuendelea kuteseka na kukosa haki za msingi.

"Serikali inaendelea na jitihada za kutokomeza ukatili wa kijinsia, lakini ombi langu kwenu wananchi muwe tayari kushirikiana na vyombo vya dola kwa kuripoti na kutoa taarifa sahihi haraka mnapoona au kusikia matukio ya ukatili yanafanyika katika maeneo yenu ili jamii iwe salama," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lidya Kwesigabo, alisema kutokana na elimu ambayo wamekuwa wakiitoa kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, ukatili wa kijinsia mkoani humo umepungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

***Imeandikwa na Vitus Audux na Marco Maduhu***

# Vijana watakiwa kuongeza uzalishaji samaki

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Wilaya ya Ukerewe mkoani hapa, Christopher Ngubiagai amewataka vijana walioijiunga na vikundi kwenye mradi wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba kuongeza ubunifu, uzalishaji na kukuza mtaji.

Ngubiagai alitoa rai hiyo juzi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda wakati wa uvunaji wa samaki tani mbili za mradi wa kikundi cha vijana Isingiti uliopo eneo la Kisoko Kata ya Luchelele jijini Mwanza.

Alisema uchumi wa bluu kwa sasa umekuwa mkombozi kwa vijana, hivyo kazi iliyopo ni kuongeza wigo na kuwasaidia kusonga mbele kwa maendeleo.

"Serikali imeweka mazingira mazuri katika sekta hii ya uvuvi na kupitia mikopo inayotolewa na Benki ya TADB, hakuna tena sababu ya vijana kukaa vijiweni badala yake ni kuchangamkia fursa hii kujiletea maendeleo," alisema Ngubiagai.

Alivipongeza vikundi hivyo kwa nidhamu ya kurejesha mikopo kwa asilimia 100 na kuleta mzunguko mzuri kwa wakopaji wengine.

Akitoa taarifa ya kikundi hicho, Katibu Omari Mangu, alisema walipewa mkopo wa zaidi ya Sh. milioni 122 na kununua vizimba vinane kwa zaidi ya Sh.milioni 33 na kupandikiza vifaranga 80,650 vilivyogharimu zaidi ya Sh.milioni 14.

Meneja wa TADB Kanda ya Ziwa, Samson Siyengo, alisema Sh. bilioni nne zimetolewa kwa vikundi hivyo mkoani Mwanza ili kuwasaidia wanachama wake kukukua kiuchumi na kuleta maendeleo katika sekta ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba.

Siyengo, alisema katika awamu ijayo watatoa Sh. bilioni tano ili kuhakikisha wanafikia kundi kubwa la vijana.

Mradi huo ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan Januari 30, mwaka huu katika Uwanja wa Nyamagana sambamba na ugawaji wa boti za kisasa zilizotolewa kwa mkopo kwa baadhi ya wavuvi wa Ziwa Victoria.

**Serikali imeweka mazingira mazuri katika sekta hii ya uvuvi na kupitia mikopo inayotolewa na Benki ya TADB, hakuna tena sababu ya vijana kukaa vijiweni badala yake ni kuchangamkia fursa hii.**

# ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI DESEMBA 12, 2024



Ukurasa 14

**Kinamama Uingereza wahamia staili mume si hitaji la lazima kupata mtoto**



**'Rafu' za wachimbaji dhahabu wadogo zinavyozitesa sekta nne**

Ukurasa 13

## MITI MIOMBO IKISHAMIRI ZAO KUU...

# Anakokanyagia Dk. Samia katika misitu, wasifu wake kimataifa na wajibu nchini

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI sasa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, sehemu ya sauti yake kila kuchao ndani na nje ya nchi anapigania afya ya misitu na mazingira.

Mara zote hutamkwa 'mtoto anavyolelewa ndivyo anavyokua'. Dk. Samia, amedumu na sauti yake kutetea mazingira akiwa uzeeni, ujanani akiwa waziri, alionekana hata msituni akitetea kwa nguvu halisi.

Mwaka 2018, akiwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani nchini ikifanyika Dar es Salaam, Dk. Samia alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya Umoja wa Mataifa, serikali na wadau wakiazimia kuendelea kushirikiana na Tanzania kupigania usalama wa mazingira.

Dk. Samia akahutubia na kutembelea maonyesho ya harakati za mbinu za kulinda mazingira, katika ujumbe wa kitaifa nchini, kupatikana mbadala wa mkaa.

Ni aina ya juhudi zikampandisha daraja, hata kufika Aprili mwaka huu katika kikao kilichofanyika nchini Marekani, Dk. Samia sasa akiwa Rais, akajikuta anapokea pongezi nyingi kwa mageuzi katika uzio wa misitu na mazingira.

Ilikuwa nchi wanachama za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zikimpongeza Rais Dk. Samia, kusimamia vema na kuhifadhi misitu ya miombo.

Pia, ikasisifika juhudi za kuhakikisha Tanzania inahama kutoka kwenye matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, ifikapo mwaka 2030.

Rais Dk. Samia akawakilishwa




katika kikao hicho na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, mwenye ufafanuzi:

"Kikubwa nchi zimeweza kumpongeza Rais wetu Dk Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa akitoa maelekezo mbalimbali kwetu sisi kama wizara na sekta.

"Kuhakikisha kwamba misitu ya miombo inalindwa kwa nguvu kubwa na kwa namna ambavyo amechukua uamuzi thabiti wa kuhakikisha kwamba inapofika mwaka 2030 zaidi ya asilimia 80 ya wananchi watakuwa wameachana na matumizi wa kuni na mkaa"

Kwa mujibu wa waziri huyo, misitu ya miombo nchini katika Ukanda wa Kusini, imekuwa ikikabiliwa na changamoto za uharibifu wa misitu unaosababishwa na ukataji miti usiozingatia sheria, taratibu na kanuni, moto, kilimo cha kuhama, uharibifu wa vyanzo vya maji na mabadiliko tabianchi.

Aidha, anafafanua kuwa kupitia mkutano huo, wadau mbalimbali wameanza kuonyesha nia ya kusaidia mpango wa utekelezaji Azimio la Maputo la mwaka 2022, kuhusu ulinzi na uendelezaji misitu ya miombo nchini.

Mkutano ulilenga kuendeleza Azimio la Maputo katika kulinda na kuendeleza misitu ya Miombo, ambayo Tanzania inagusa takriban asilimia 93 ya misitu Tanzania, inatunza wanyamapori, vyanzo vya maji na huduma za kijamii.

Kamishna Uhifadhi wa Wakala ya Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo anasema kupitia Mkutano huo wa nchi za SADC, zimekuwa zikijadili namna ya kushirikiana kwa nchi na wadau wa maendeleo kupata rasilimali fedha, kukuza ujuzi na utaalamu.

Katika mwendelezo wa matukio, Rais Dk. Samia, Agosti mwaka huu akiwa mgeni mwalikwa katika taasisi ya TFS, Kusini Unguja, alikagua zao jipya la 'utalii wa nyuki'; hata likaibua shauku na kuvutia watu wengi.

**MTAZAMO ULIVYO**

Serikali imekuja na mkakati mwarobaini wa kutokomeza ukataji miti ovyo, kwa ajili ya matumizi ya kupika majumbani kwa mkaa na kuni; hali hiyo sasa imegeuka utamaduni katika jamii mijini na vijijini.

Kwa vijijini, idadi kubwa ya wananchi wamekuwa wakitumia kuni kwa matumizi yao ya kila siku, ama kwa kukata au kutoka miti inayoanguka.

Matumizi ya mkaa kwa kiwango kikubwa yameteka maeneo ya mijini, ambako hakuna mashamba ya miti na misitu iliyotengwa mahsusi kwa hifadhi za kiserikali.

Iko bayana, ukataji miti kwa kiwango kikubwa unachagizwa na biashara ya mkaa katika maeneo ya mijini, kuna watumiaji wakubwa kwa ajili ya kupikia majumbani.

Watumiaji ni wafanyabiashara wa mahindi ya kuchoma, nyama na wafugaji kuku wa kisasa kwa ajili ya kuweka joto kwenye mabanda yenye vifaranga dhidi ya baridi.

Kutokana na kuendelea kasi ya ukataji miti katika maeneo nchini, serikali nayo imesimama kidete kupinga vitendo adha hiyo, sasa ikianzisha kampeni, pia kutunga sheria dhidi ya wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Vilevile, kumekuwapo taasisi zinazojihusisha na kuhifadhi, pia kutunza mazingira hususani miti, ili kuondokana na tishio la baadhi ya maeneo kugeuka jangwa.

Madhumuni ya taasisi hizo yana lengo la kuisaidia serikali kufanikisha kampeni zake, kupiga vita ukataji miti ovyo kwa matumizi ya kupikia majumbani, hata mbao bila ya kuwa na vibali.

Wajibu uliofika sasa ni kwa serikali, pia taasisi hizo zinatakiwa kuwa na mawasiliano, ili nchi

Inaendelea Uk. 12

AFYA

## UKIPATA SHIDA HULALI...

# Watafiti wabuni jibu, orodhesha yote unayoyawaza kufanya, utasinzia tu!

• Njia sahihi; karatasi au simu...endelea kuchati

**Na Mwandishi Wetu**



Mtu aliyeaacha usingizi, kisha kuorodhesha mambo yanayomuumiza kichwa. **PICHA: MTANDAO.**

WATAALAMU sasa wamekuja na jibu, kwamba ikitokea una tatizo la kupata usingizi, basi suluhisho ni haraka kuwa na kalamu na karatasi, ukayaoorodhesha.

Utagundua kinachokunyima usingizi ni kufikiria sana mambo ambayo unatarajia kuyafanya siku inayofuata, hasa kazi ambazo umeanza na hujamaliza.

Katika utafiti uliofanywa na wafanyakazi katika kampuni ya Teknolojia na Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya Ujerumani, waliokuwa na kazi hazijakamilika mwishoni mwa juma la kazi, walikuwa na uwezekano wa kufikiria matatizo yao ya kazi mwishoni mwa juma, ikilinganishwa na ambao hawakuwa na kazi nyingi walizobakisha.

Mtafiti Christine Syrek kutoka Chuo Kikuu cha Trier, akaandika ni matokeo yaliyoonyesha "hali ya kutokamilisha kazi za wiki huathiri afya ya wafanyakazi na kusababisha kutopata usingizi hasa wikendi, pia athari za kutokuwa na muda huchangia hili".

Anasema 'mwendelezo wa kiakili"ni kufikiria sana mambo mabaya yaliyowahi kukutokea au unatarajia yatokee siku za usoni. Watu wakiwa katika hali hii pia hujipata wakitatizika kupata usingizi wa kutosha katika likizo ya wikendi.

Kuandika mambo unayotarajia kufanya siku ifuatayo kutakufanya upate usingizi kwa haraka,utafiti waonyesha; Usiku wa Jumapili huwa una changamoto zake.

Iwapo una shughuli asubuhi inayofuata, unaweza kukosa usingizi. Unawaza majukumu unayotarajia kuyatekeleza na mapya ambayo pia hujayamaliza.

### CHA KUFANYA

Je ni kipi unapaswa kufanya ili upate usingizi mnono na kutofikiria sana? Jibu, ama usome kitabu kwa muda ,au ufikirie mambo ambayo hayazunguki mazingira yako ya kawaida. Unawaza ukiwa makini na kusikiliza mapigo ya moyo wako na hisia zinazokuzunguka.

Ama uamke na uandike mambo yote unayotarajia kufanya siku ifuatayo ili akili itulie.

Yamkini, hatua hiyo ya kuorodhesha unayopanga kuyafanya husaidia sana na baada ya utafiti kufanywa Marekani na kubainika husaidia kutuliza ubongo na kupata usingizi kwa haraka.

Mkurugenzi wa Maabara ya Neuroscience na Utambuzi wa Usingizi katika Chuo Kikuu cha Baylor nchini Marekani, Michael Scullin, aliuliza kikundi kimoja cha watu waliojitolea kuandika orodha kabla tu ya kulala ya kila kitu ambacho wamefanikiwa kufanya.

Pia, katika kikundi cha pili kuandika orodha, kuhusu kazi walizopaswa kufanya kukamilisha majukumu yao hapo kesho, ni kundi la pili ambalo baadaye lilipata usingizi kwa haraka zaidi.

Badala ya kuwa na kazi zinazozunguka kichwani mwako bila mpangilio, zinawekwa mpangilio wa aina fulani.

Wanasayansi hawakutegemea tathmini ya watu waliojitolea kuhusu usingizi wao (ambao si sahihi kila wakati), lakini ilithibitishwa walipokuwa wameamka na kulala kupitia aina ya utafiti wa usingizi unaojulikana kama 'polysomnografia.'

Hiyo inahusisha kuambatisha vitambuzi kwenye kichwa cha mtu na sehemu nyingine za mwili ili kufuatilia mawimbi ya ubongo, kupumua na mienendo yao.

Kushughulikiwa kwa wakati unaofaa. Kama bonasi sio lazima kuwa na wasiwasi juu ya kuzisahau.

Hapo kuna utaratibu wa kisaikolojia ambao unaweza kueleza kwa nini alipata matokeo aliyoyafanya inaitwa "cognitive offloading" na hutokea wakati mtu anachukua hatua ya kimatendo ili kupunguza mzigo wa akili.

Unaondoa baadhi ya kazi ya kiakili unayohitaji kufanya ili kujieleza, na hivyo kupunguza mkazo kwenye ubongo wako na kufanya kazi ya kwenda katika mwelekeo sahihi iwe nafuu.

Kuandika mambo unayotaka kufanya kwa karatasi inafahamika kama"kupunguza mambo akilini" Kwa upande wa orodha iliyoandikwa ya mambo ya kufanya kesho yake kabla ya kulala, unapakua majukumu yako kutoka akilini mwako hadi kwenye kipande cha karatasi au simu ukipenda.

Na ikiwa una uhakika hutavutiwa kwenye mitandao ya kijamii au yako, tumia barua pepe kwa njia ambayo inapunguza hitaji la wewe kuzifikiria unapojaribu kulala.

Hiyo ni badala ya kuwa na kazi zinazozunguka kichwani mwako bila mpangilio, zinawekwa katika mpangilio wa aina fulani.

Zinahifadhiwa, kana kwamba ziko tayari kushughulikiwa kwa wakati unaofaa. Ufanisi unaokuwa nao ni hutakuwa na muda wa kufikiria sana iwapo utasahau.

Ni vyema kuorodhesha majukumu mahususi, badala ya kuandika kwa ujumla, ingawa itafanya orodha yako kuwa ndefu zaidi.

Utafiti wa Profesa Scullin, uligundua kuwa watu wenye shughuli nyingi ambao waliunda orodha ya kazi zaidi ya 10 walilala kwa wastani wa dakika 15 haraka kuliko watu ambao hawakuandika orodha za kazi.

Pia, walilala kwa dakika sita haraka kuliko wale ambao walikusanya orodha fupi tu. Kwa hivyo, fanya kuwa pana.

Kufanya hayo yote kunaweza kuonekana kama kazi ngumu wakati umechoka na unajipanga kulala. Lakini inaweza kuwa na thamani yake.

Kuandika orodha yako ya mambo ya kufanya kabla tu ya kuingia hakutafanya maisha yako kuwa na shughuli nyingi, lakini kunaweza kukusaidia tu kupata usingizi na kuwa na wasiwasi kidogo.

Na ukiamka siku inayofuata, tayari umejipanga kwa sababu unayo orodha ya kila kitu unachohitaji kufanya siku hiyo.

• ***Kwa mujibu taarifa kimataifa.***

## ANAKOKANYAGIA DK. SAMIA KATIKA MISITU, WASIFU WAKE KIMATAIFA NA WAJIBU NCHINI

**Inatoka Uk. 11**

iweze kufanikisha malengo yake kwa manufaa ya wananchi na vizazi vijavyo katika hatima ya misitu.

Kwa ujumla, taasisi hizo zinatakiwa kufanya kazi kama timu na siyo kila moja kivyake katika kufanikisha maono ya taifa katika uhifadhi wa mazingira.

Hapo kuna nafasi nyingine ya maofisa misitu, waendeshaji mashauri mahakamani, viongozi wa serikali za mitaa, vijiji kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza miti na kuhifadhi mazingira yao kwa manufaa yao.

Ni dira inayotarajiwa kuondoa changamoto za kukosa hewa safi, kudhibiti magonjwa na kufahamu sheria za ulinzi misitu kitaifa.

Tayari kuna nchi duniani zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kukabiliana na changamoto za kukosa mvua, lakini baada ya wananchi wake kupatiwa elimu na kutumia sheria kali dhidi ya wanaokiuka.

Ni wakati unatajwa kwa Tanzania kuhimiza wananchi kutunza misitu, wafanyabiashara ya mkaa na kuni, kubuni biashara mbadala wa kuwapatia kipato cha kujikimu kimaisha.

Hiyo inaendana na serikali kudhibiti taasisi zinazotoa vibali vya kukata miti, badala yake kuzama katika kudhibiti ukataji miti ovyo, ikiendana na kampeni ya matumizi ya nishati safi ya gesi kupikia nchini ikidhibiti ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa.

Kampeni hadi sasa inaendelea katika mikoa mbalimbali nchini, kuongeza idadi ya watumiaji gesi za kupikia majumbani na sehemu za biashara, zikiwamo kwa mamalishe na babalishe.

### MSINGI WA UTAFITI

Utafiti uliofanyika nchini mwaka 2020 unaonyesha idadi kubwa ya wananchi wapatao asilimia 63.5 wanatumia kuni kupikia, 26 mkaa tano gesi.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, nishati safi ya kupikia bado ni changamoto katika jamii, hivyo kampeni hiyo iliyoasisiwa na Rais Samia Suluhu Hassan kumtua kuni mwanamke kichwani, inatakiwa iendane na elimu katika jamii kumletea mafanikio makubwa.

Mafanikio hayo ni pamoja na kutokomeza magonjwa yanayosababishwa na hewa ya ukaa, kutokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mengine ni kutunza, kuhifadhi misitu na kupata mvua za kutosha nchini na kuokoa muda wakati wa kupika na jamii kufanya shughuli za uzalishaji mali.

MAZINGIRA

# ‘Rafu’ za wachimbaji dhahabu wadogo zinavyozitesa sekta nne

- Wachimbaji: Bila kukata miti hatuifikii
- Wakikosa madini, wanavamia mti mkaa
- Wafugaji nao kundi linaloumiza vichwa

**Na Ibrahim Yassin, Songwe**

KUKITHIRI kwa uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji katika bonde la Ziwa Rukwa, sasa katika kunahitaji ushirikiano wa zaidi ya sekta tatu kudhibiti, Nipashe limebaini.

Uharibifu huo wa mazingira unafanywa hasa na wafugaji na wachimbaji madini ya dhahabu ambao baadhi yao wamekuwa wakitiririsha maji yenye kemikali kwenye mito na wengine wakikata miti ovyo na kuharibu uoto wa asili.

Baada ya Nipashe kupata taarifa za uharibifu huo na kuchunguza katika bonde la Ziwa Rukwa, imebainika kuwa sekta zaidi ya tatu zinahitajika ili kupanusuru.

Imebainika kuwa uharibifu mkubwa unaofanywa na wachimbaji wa dhahabu katika bonde hilo, sasa unahatarisha kutoweka miti ya asili na uoto wake kwenye vyanzo vya maji.

Hapo pana ushuhuda katika vyanzo vya mito ya Lupa, Tete, Zila, Kipoka, Mbuzi, Kalungu, Saza, Lwika, Kilinga na Mto Mlamba Ng'ombe, ambako shughuli za uchimbaji zinaendelea kwa kasi na kuharibu vyanzo vya maji pamoja na mazingira.

Imefahamika mito kama Zila, Lwika na Lupa ndiyo yenye samaki, lakini kutokana na wachimbaji kufanya shughuli za uchimbaji hadi ndani ya mto, kumefanya mito hiyo kuondokewa na uoto, hata mito ya asili.

Utafiti umebaini kuwa elimu kwa wachimbaji hao haijawafikia zaidi ambapo elimu zaidi inahitajika kutolewa na sekta zote ili waweze kutambua umuhimu wa kutunza mazingira.



Sehemu ya mfumo kuingia shimoni kunakochimbwa dhahabu mkoani Songwe.

**WADAU WAFUNGUKA**

Mchimbaji anayejitambulisha kwa jina la Hussein, anayefanya shughuli zake katika maeneo ya Saza wilayani Chunya, anasema kuwa suala la mazingira ni magumu kuzingatiwa, kutokana na wao wachimbaji katika maeneo wanakofanyia kazi, lazima wakate miti, ndio wafanikishe lengo la kuchimba.

Hussein anasema, hata wanapotakiwa kuingia ndani ya shimo ambalo limekuwa refu, lazima watumie miti ambayo ni migumu kuzuia mmomonyoko wa udongo.

"Sisi tunaangalia pesa, kama ni masuala ya mazingira tukishachimba tunawachia maeneo yao 'tunasepa' zetu," anasema Hussein.

Katika hilo la uharibifu wa mazingira katika bonde hilo, Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Ziwa Rukwa, Mhandisi Jackson Waled, anasema suala hilo linahitaji sekta zote nne zinazohusika moja kwa moja na uharibifu wa mazingira kwenye bonde hilo.

Waled anazitaja kuwa sekta za: Madini, Mifugo, Kilimo na Maliasili na kwamba zinapaswa kuweka mikakati ya pamoja kudhibiti uharibifu tajwa wa mazingira katika bonde hilo, ili kurudisha uoto wa asili uliotoweka, ikiwamo kingo za mito zilizomeguka.

Mkurugenzi huyo anasema, tatizo kubwa lililopo ni uwapo wa wachimbaji madini hadi kwenye vyanzo vya maji licha ya elimu za mara kwa mara wanazopewa, lakini kumekuwapo changamoto za kuwadhibiti.

Anasema, tatizo linalofanya washindwe kuwadhibiti ni kutokana na wachimbaji kuhama kila mara na wanaingia wapya ambao hawajapatiwa elimu sahihi.

Ni utaratibu unaohusu pia, umuhimu wa kupatikana leseni, pale mchimbaji anapokuwa kapatiwa elimu kunusuru uharibifu zaidi.

Anaendelea: "Licha ya kutoa elimu kwa baadhi ya wananchi walioko kwenye maeneo hayo. Shida iliyopo ni wachimbaji wageni kuingia kwenye maeneo, pasipo kupewa elimu hiyo. Tukiungana sekta zote (kudhibiti hilo), tutafanikisha."

Mkurugenzi huyo anaendelea kuwa, kwa sasa serikali inawahimiza wachimbaji kupata lesseni, pale tu wanapokuwa wamepewa elimu ya umuhimu wa kutunza mazingira.

Waled anaongeza kuwa baadhi ya wachimbaji wanapokosa dhahabu, hugeukia kukata miti na kuchoma mkaa, jambo linalochangia kuharibu mazingira ya nchi.

Anasema kuwa hata wafugaji nao wamekuwa wakichunga kwenye vyanzo vya maji na kuharibu uoto huo wa asili.

Hapo anafafanua kwamba, kuwapo mifugo mingi kwenye vyanzo vya maji, nako kumechangia kuharibifu mazingira husika, pale mifugo inaingizwa kwenye mito na kusababisha kingo kubomoka.

Anasema, mifugo mingi inachangia kulainisha mchanga au udongo kwenye vyanzo vya maji, pia anasema hata mchanga unaochimbwa, pale mvua zinaponyesha, unazama kwenye mito na kupunguza kina cha mto, hata kufanua maji ya mto yakasambaa.

Mkurugenzi anataja moja ya jitihada wanazozifanya, ni kuunda jumuiya za wananchi walioko kwenye maeneo hayo, kusaidia kutoa elimu kwa wenzao.

Anasema jumuiya hizo zimekuwa zikiwezeshwa kwa kupewa elimu ili nao waweze kufundisha wenzao umuhimu huo wa kutunza mazingira.

**KIONGOZI WA WACHIMBAJI**

Mwenyekiti Mstaafu wa Wachimbaji Mkoa wa Songwe, Emmanuel Kamaka, anasema, wachimbaji huwa wanapewa elimu, lakini tatizi liko katika mustakabali wa kazi yao akieleza “ni kwamba lazima baadhi ya vitu, vitahusika kuviharibu kama miti na mito.”

Anasema, dhahabu zinapatikana kwenye miamba ya mawe, ambayo yapo porini kwenye miti mingi, hata kuleta ugumu wa kuchimba bila ya kufyeka baadhi ya miti hiyo.

Anasema, hata kwenye mito kuna baadhi ya dhahabu zinapatikana kwenye maji, akitaja kwa jina ‘Arruvial Gold’ isiyohitaji gharama kubwa kuchenjuliwa.

**WATAALAMU SERIKALINI**

Ofisa Kilimo Wilaya ya Chunya, Cuthbert Mwinuka, anasema kuwa elimu imekuwa ikitolewa kwa wakulima, isipokuwa tatizo liko katika mwingiliano baina ya wafugaji na wakulima.

Anawataja wafugaji na wakulima, nao wamekuwa miongoni mwa wanaoharibu mazingira, hata wanachukua hatua ya kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.

Kwa upande, Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Chunya, Benedict Matogo, anasema wafugaji wamekuwa wakipewa elimu ya kutunza mazingira na ndio maana wamepangiwa maeneo yao ya kuchunga.

Anasisitiza kuwa, suala la mazingira linahitaji jitihada za pamoja kijamiii, ikiwamo mchango wa wanahabari kuelimisha utunzaji mazingira.

Matogo anasema, sekta moja haiwezi kukamilisha kuzuia uharibifu wa mazingira, hivyo ni lazima Watu wa Kilimo, Madini, Maliasili na Mifugo wajidhatiti kutoa semina elekezi kwa wananchi wao.

**SURA YA MADHARA**

Uharibifu wa mazingira, unatajwa kimataifa kuwa uzoroteshaji wa mazingira kwa njia ya kupunguza rasilimali kama vile hewa, maji na udongo na kupotea wanyamapori, huku maliasili ikitumiwa vibaya.

Inasisitizwa kuwa, uharibifu wa mazingira ni moja ya vitisho 10 vinayotolewa tahadhari na Umoja wa Mataifa, Shirika la Rasilimali Duniani, pia Benki ya Dunia, kupitia Ripoti ya Afya na Mazingira Duniani ya Mwaka, 1998.

Katika maeneo maskini duniani, inakadiriwa hatari kuwa mmoja katika watoto watano hawataishi kuona siku yao ya kuzaliwa ya tano, hasa kwa sababu ya magonjwa yanayohusiana na mazingira.

Vilevile inatajwa wastani wa watoto milioni 11 duniani kote hufa kila mwaka, wakiunganishwa hasa na maradhi kama malaria, shida za kupumua na kuhara, shida zinazotajwa zinazuilika.

Majumuisho ya madhara hayo hubeba tafsiri ya kusababishwa vifo, hivyo nguvukazi ya taifa inapungua na kukwamisha maendeleo ya taifa, hata inaangukia changamoto kubwa kijamii.



Sehemu ya misitu inayosambaratishwa, kusaka madini mkoani Songwe. **PICHA ZOTE: IBRAHIM YASSIN.**

AFYA

# Kinamama Uingereza wahamia staili mume si hitaji la lazima kupata mtoto

## •Kinachowaumiza kichwa 'nitamleaje?'

**Na Mwandishi Wetu**



Watoto wenye mzazi mmoja nchini Uingereza, wakifurahia na mama zao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Una upendo na usaidizi karibu nawe, kwanini ungojee mwanaume?" Pata simulizi:

HADI sasa duniani kuna wanawake wasio na waume wanapitia suala la upandikizaji mbegu, nchini Uingereza wakimea zaidi na njia hiyo inayoitwa IVF, imeongezeka zaidi ya mara tatu katika muongo mmoja.

Hiyo ni kwa mujibu wa takwimu mpya, ikitaja kati ya miaka 2012 na 2022, ripoti inaonyesha idadi ya wanawake walio na matibabu ya uzazi ilipanda kutoka 1,400 hadi 4,800.

Kuna wataalamu na wanawake waliopanga maisha ya kuwapo mzazi mmoja, wakisema wanawake wengi zaidi wanaoamua kutokuwa na watoto hadi wanapokuwa wanapata wenza wao, ni miongoni mwa yanayochochea ongezeko hilo.

Lakini wengi bado wanakabiliwa na vikwazo vya kifedha wakati wa kupata matibabu na katika uzazi huo wa pekee.

Kinamama waliaomua kuanzisha familia yao wenyewe ana hoja zao, mmojwapo ni Gina anayesema kwa mara ya kwanza alianza 'kwa umakini" kufikiria hilo, kuwa mama asiye na mume.

Anasema, baada ya kufanyiwa tathmini ya uzazi katikati ya miaka yake ya 30na kupatiwa matokeo, aliwajuza kwa kauli: "Sawa, uzazi wangu ni mzuri kwa umri wangu ... hili ni jambo ambalo nataka kufanya".

Gina anaendelea: "Nilikuwa kwenye mahusiano mara kwa mara, lakini nilihisi kama ni afadhali kufanya hivyo peke yangu kuliko kuwa katika uhusiano na mtu kwa muda mrefu."

Anaendelea "na kufikiria ikiwa unataka kuwa na watoto naye au la na kama wakati wako umekwisha na kama unaishia kuwa mzazi asiye na mwenzi."

Muuguzi wa Afya ya Akili katika jamii, alipitia upandikizaji wa ndani ya uterasi (IUI) kwa kutumia mbegu za wafadhili.

Ni matibabu ya uwezo wa kuzaa ambayo yanahusisha kuingiza mbegu moja kwa moja kwenye tumbo la uzazi. Iligharimu takribani pauni 1,500 na alipata ujauzito mnamo 2021 (sawa na shilingi 3,655,080.00 ya sasa).

Anasema, amekuwa na mtandao wa karibu wa familia, huku dada yake akihudhuria kliniki kumfuatilia na mama yake akiwa mshirika wake wakati wa kujifungua, Gini anasimulia hakumbuki kuwa na wasiwasi wowote kuhusu matarajio ya mzazi mmoja.

"Kuyafanya haya kwa masharti yangu mwenyewe kulinifaa," anaongeza, akisema tangu awe na mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka miwili sasa, amehama makazi kutoka Yorkshire akarudi nyumbani kwao, Northumberland.

Ni uamuzi wenye maana ya kumsaidia kukabiliana na shinikizo na gharama za malezi ya Watoto,a akikiri upande wa pili, kwamba: "Kuna wakati wake, inaweza kuwa ngumu,"

"Lakini ninaendelea tu na mambo kwa sababu sina mtu mwingine wa kunikatisha tamaa," anasema na kuongeza:

"Ikiwa uko mahali katika maisha yako ambapo unataka kuwa na mtoto na una upendo na usaidizi karibu nawe, kwanini ungojee mwanaume?"

### YAKE MAMA SOPHIE (46)

Mama Sophie (46), anatumia zaidi ya miaka yake 30 akinena ni "maisha ya kufurahisha na yenye furaha."

Anasema, aliamua kujaribu kupata mtoto peke yake, mwanzoni kupitia mfumo uitwao 'IUI', lakini akaupoteza ujauzito.

Kisha akagandisha mayai yake na kuamua kupitia mfumo 'IVF' peke yake na alipopofaulu mwaka 2021, Sophie, aliyetumia panui za Uingereza 30,000 (Sh. 100,632,680.25) katika mchakato mzima, anajiona fahari sasa.

Wakati wa ujauzito wake, katika hatua za awali za uzazi wa Sophie, anasema: "Hakuwahi kuwa na hofu na hakika hana majuto yoyote".

Anasema wengine walikosoa uamuzi wake, akiwapo mshauri wake, aliyemwambia "unaleta mtoto ulimwenguni ambaye atakuwa na mzazi mmoja tu. Itakuwaje mzazi huyo akifa?

"Niliheshimu maoni yake kabisa, lakini najua sasa kwamba Martha (mtoto) ana umri wa miaka mitatu na tuna uhusiano wa pekee sana. Ana maisha thabiti," Sophie alisema.

Ingawa tayari amemweleza mwanawe aitwaye Martha jinsi alivyotungwa mimba, Sophie anasema ataendelea kuwa "wazi kuhusu kila kitu" kadiri uelewa wake unavyoongezeka.

Anaongeza kuwa uzazi wa pekee aliopanga ulikuja na matatizo.

"Unafanya maamuzi yote wewe mwenyewe, unajisumbua mwenyewe, huna mtu wa kupeana naye mawazo lakini.... unatambua jinsi ulivyo na nguvu wakati mtoto anaumwa na haujapata usingizi," anasema.

### MAMA WAWILI MICHELLE (42)

Safari ya Michelle kupata watoto wawili kupitia IUI kwa kutumia mtoaji mbegu za kiume, ilianza baada ya kumalizika kwa uhusiano na mwanaume.

"Nilikuwa na mpenzi kwa muda mrefu na siku zote, nilijua nilitaka kupata watoto. Alikuwa kwenye uzio kuhusu kufanya hivyo," anasimulia Michelle na kuendelea:

"Uhusiano huo ulipoisha, nilihisi 'nina umri wa miaka 38 sasa (wakati anaamua), sina wakati wa kupata mtu na kuruhusu uhusiano huo kukua kwa njia ya asili."

Badala ya kusitasita kutafuta mtoto, Michelle akaamua kuacha kuwa na uhusiano naye na akaingia katika mbadala wa kulipa pauni za Uingereza1,800 (Sh.5,966,617.68) kwa IUI kwa kutumia mtoaji mbegu na akapata mimba.

Kabla ya kujifungua mtoto wake wa kiume mwaka 2021, alikwenda kukaa na mama yake kwa muda mrefu akinena: "Kuna mambo mazuri na mabaya ya kuifanya na mshirika au bila. Kila kitu kiko kwenye mabega yako, huwezi kupata kahawa na rafiki yako bila mtoto."

Mnamo mwaka 2023, akapata binti kupitia njia ile ile ya kupata mimba, leo hii watatu hao sasa wanaishi Pamoja.

### CHANGAMOTO ZILIZOKO

Ingawa kumekuwapo ongezeko kubwa la idadi ya wanawake wasio na waume wanaopata matibabu ya uzazi ili kupata mimba, idadi bado ni ndogo.

Kuna vikwazo vya wazi vya kifedha kwa njia hii ya uzazi. Hiyo haitolewi kila mtu, bali kwa wengi ni pale kunakuwapo nafasi ya kufanikiwa kupata ufadhili, kulingana na pale mhitaji anaishi huko Uingereza.


Majorani zao, Scotland hawafadhili matibabu ya uzazi kwa wanawake wasio na waume. Lakini katika maeneo mengi, wanawake wanapaswa kulipia angalau 'mizunguko sita ya upandikizaji' kitaalamu, kabla ya kukubaliwa na ndio ufadhili unapoanza

Mtaalamu Dk, Hill pia anataja vizuizi vya kifedha kulea familia peke, huku zikizidi kupanda nchini Uingereza.

"Wanawake wasio na waume wanaochagua IVF au upandikizaji ni mwelekeo unaokua," anasema, akiongeza kuwa wanawake ambao walitaka watoto walikuwa wanazidi kufahamu 'vizuizi' vyao linapokuja suala la uzazi, na wanazidi kulichukulia suala hilo mwenyewe.

Wakati huo huo, Dk Hill.anataja unyanyapaa nao unatajwa kupungua, akinena: "Nadhani mitazamo ya kijamii imebadilika kuhusu akina mama wasio na waume na nadhani kinachohitajika sasa ni sera kuafiki mabadiliko hayo."

***Kwa mujibu wa BBC***







## Mavunde atekeleza ahadi, awajengea nyumba watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde ametekeleza ahadi yake ya kuwajengea nyumba watoto ambao mama yao alifariki kwa kudondokewa na ukuta wa nyumba waliyokuwa wakiishi Mtaa wa Nguji, Mbabala jijini Dodoma.

Miaka miwili iliyopita ilinyesha mvua kubwa na kusababisha maafa ikiwemo kuharibu mali na baadhi ya wananchi kupoteza maisha akiwamo mama huyo na kuacha watoto wawili Baraka na Hamisi Ijinji.

Akizungumza jana alipokuwa akikabidhi nyumba hiyo, Mavunde ambaye ni Mbunge wa Dodoma Mjini, alisema watoto hao Hamis na Baraka walipatwa na kadhia hiyo ya kudondokewa na nyumba ambayo ilipoteza maisha ya mama yao na wao kuokolewa na wasamaria wema.

"Nilipotembelea waathirika wa mafuriko kwenye eneo hili, nilikutana na jambo ambalo lilinigusa lilikuwa linahusisha watoto wawili wadogo kwenye nyumba waliyokuwa wakiishi na mama yao kubomoka."

"Niliahidi kuwajengea nyumba watoto hawa ili kuwasaidia kupata makazi yao ya kudumu,namshukuru Mungu leo nimekamilisha ahadi yangu na nimekabidhi nyumba hiyo na nitaendelea kuwasimamia kwa mahitaji yao muhimu kwa kadri Mungu atakavyoisaidia,"alisema.

Aliomba jamii kusimamia malezi ya watoto hao kwa karibu ili wafanye vizuri kwenye masomo yao na kuendelea na hatua nyingine za elimu.

Mlezi wa watoto hao, Mchungaji Lazaro Peter alimshukuru Mavunde kwa kutimiza ahadi na kuwafariji watoto hao kwa kuwaboreshea makazi na kuahidi kuendelea kuwasimamia watoto hao katika malezi bora ili watimize ndoto zao.

Alisema kwasasa watoto hao wanaendelea na shule ili wafikie ndoto yao kielimu.

Diwani wa Kata ya Mbabala, Paskazia Mayala alimpongeza Mavunde kwa kuwa karibu na kuwajali watu wenye mahitaji kama alivyofanya kwa watoto hao.

# Mradi wa maji kuleta neema wakulima 2,000 Kijiji Membe

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) inatekeleza mradi wa mkakati wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji wa lita bilioni 12 katika Kijiji cha Membe wilayani Chamwino, mkoani Dodoma itakayonufaisha wakulima 2,000.

Mradi huo wa Sh. bilioni 16.2 na wakulima hao watajikita kuzalisha mazao mbalimbali ya kiuchumi na chakula katika shamba la ekari 7,500.

Akizungumza jana na Nipashe, mhandisi wa mradi kutoka NIRC, Salehe Ramadhani alisema utekelezaji wa ujenzi wa skimu hiyo kwa sasa umefikia asilimia 86.

Alisema fedha za mradi huo zimetolewa na serikali na unatekelezwa na kampuni ya mkandarasi mzawa ya Nakuroi Investment Company Ltd.

**Kama kampuni ya ndani, tunaishukuru sana serikali kwa kutupa zabuni hii kubwa ya kitaifa. Utekelezaji wa mradi huu umetoa fursa za ajira kwa wazawa wengi wa Kijiji cha Membe.**

"Utekelezaji wa mradi huu ulianza Septemba Mosi 2022, na kwa makubaliano yaliyowekwa mkandarasi alipaswa kukabidhi mradi Desemba lakini kwa sababu ya mwingiliano usio wa kirafiki wa hali ya hewa,"alisema.

Mhandisi Ramadhani alisema kwa sasa mkandarasi anatakiwa kukamilisha mradi huo ndani ya miezi miwili ijayo na amelipwa zaidi ya Sh. bilioni 10.4.

Alifafanua, mradi unahusisha ujenzi wa tuta la bwawa lenye urefu wa mita 4.90, na upana wa juu wa mita sita, pamoja na kina cha wastani cha mita 14, urefu wa bwawa ni kilomita 4.5 na mita za ujazo milioni 12, ambapo ujazo wa maji ni lita bilioni 12.

Kadhalika, alisema mbali na kuhudumia kilimo cha umwagiliaji mradi huo umebuniwa kwa ajili ya kuwawezesha walengwa kufanya shughuli za uvuvi, pamoja na kupata maji ya kutosha kwa kuhudumia mifugo yao.

Mhandisi wa mradi huo kutoka kampuni ya Nakuroi Investment Ltd, Masoud Chembe alisema wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha ujenzi wa mradi unakamilika kwa viwango na kwa muda uliowekwa, Ili kuakisi thamani ya fedha zilizowekezwa na serikali.

"Kama kampuni ya ndani, tunaishukuru sana serikali kwa kutupa zabuni hii kubwa ya kitaifa. Utekelezaji wa mradi huu umetoa fursa za ajira kwa wazawa wengi wa Kijiji cha Membe," alishukuru.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka NIRC, Mariamu Mziwanda, alisema tume hiyo pia inatekeleza miradi mingine ya aina hiyo katika maeneo ya Ndogoe na Chinan'gali II mkoani Dodoma.

Alisema lengo ni kuwawezesha wakulima kuzalisha angalau misimu mitatu kwa mwaka, maendeleo ambayo yanalenga kuongeza usalama wa chakula nchini, pamoja na pato la taifa.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia kuongeza mgawo wa bajeti kwa tume kutoka Sh.bilioni 17 hadi kufikia zaidi ya Sh.bilioni 400.

Pia alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Raymond Mndolwa kwa kuisimamia tume hiyo kwa weledi na mafanikio makubwa.




Wakili wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Neema Ahmed (kushoto), akizungumza na wakazi wa Matumbulu na Mpunguzi, wakati wa maadhimisho ya siku ya kupinga ukatili yaliyofanyika kwa kushirikiana na Ushirika wa Wakulima wa Zabibu na Masoko Mpunguzi (UWAZAMAM), jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC: Nishati safi ya kupikia itapunguza vitendo vya ukatili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema matumizi ya nishati safi ya kupikia yatasaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake vijijini.

Senyamule alisema hayo juzi wakati akifunga kilele cha Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kilichofanyika jijini hapa kwa uratibu wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma pamoja na wadau mbalimbali.

"Tunapaswa kumuunga mkono Rais Samia kwenye agenda yake ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kusaidia kimama wa vijijini ambao wamekuwa wakikumbwa na madhira mbalimbali ikiwemo vitendo vya ubakaji wakiwa wanatafuta kuni za kupikia porini."

"Kuna matukio ambayo yamekuwa yakitokea wakati mwingine unajiuliza waliofanya kama ni binadamu kweli unakuta bibi kizee kabakwa hadi kufa porini wakati akitafuta kuni sasa matumizi haya ya nishati safi yatasaidia kupunguza hali hii,"alisema.

Aidha, alipongeza serikali kwa jitihada ambazo imeendelea kufanya ili kusaidia kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia ikiwemo ujenzi wa shule pamoja na mabweni karibu na jamii.

Kadhalika, alisema katika Mkoa wa Dodoma licha ya kutokea kwa matukio mfululizo ya vitendo vya ukatili wa kijinsia lakini kwa mujibu wa takwimu matukio hayo yamepungua ukilinganishwa na miaka miwili iliyopita.

"Kuna matukio yalitokea hivi karibuni kwenye mkoa wetu ikiwemo lile la baba kumnajisi mtoto wake wa miezi sita hadi kufa yalikuwa ni matukio ambayo yalileta taharuki lakini siyo kwamba mkoa ndiyo unamatukio mengi kiasi hicho,"alisema

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia bado yapo hivyo ipo haja ya wadau pamoja na serikali kuendelea kushirikiana kukomesha hali hiyo.



# Wakurugenzi wa miji waagizwa kuwabana makandarasi wa maji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKURUGENZI wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira mkoani Njombe wametakiwa kusimamia kwa karibu makandarasi wanaotekeleza mradi wa maji wa miji 28, ili uweze kukamilika kwa wakati na kuweza kutoa huduma kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Mathew alitoa agizo hilo juzi wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe.

Alisema ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati uliopangwa ni lazima wasimamizi kuongeza nguvu kwa kushirikiana na ofisi za mikoa pindi makandarasi wanapoleta uzembe.

**Miradi hiyo imeweza kunufaisha wakazi zaidi ya 177,989 hii ni sawa na asilimia 20 ya wakazi wote 889,946 waliopo katika Mkoa wa Njombe.**

"Lakini tunafahamu pia kuna miradi mingine ambayo pia ratiba yake kimkataba inatakiwa kuisha mwaka 2026 na ukiangalia jinsi ilivyo inaendelea vizuri na tutaendelea kusukuma kwa sababu kuna maeneo mengine kwenye miji 28 kabla ya mradi haujakamilika tayari wanaanza kuutumia yale maji," alisema Mhandisi Mathew.

Alisema ni matamanio ya Rais Samia Suluhu Hassani kuhakikisha miradi yote ya kimkakati ikiwemo wa miji 28 inakamilika ifikapo mwaka 2025.

"Kabla ya kukamilisha mtandao wa kila sehemu inawezekana kuna sehemu wanaweza wakaanza kunufaika na mradi wakati ujenzi unaendelea hata ukiwaambia wananchi kwamba mradi umefikia asilimia fulani lakini huduma wanapata," alisema Naibu Waziri Mathew.

Pia, alisisitiza kulindwa kwa vyanzo vya maji kwa kuhakikisha elimu inatolewa kwa wananchi wa maeneo husika sambamba na utunzaji wa miundombinu ili isiharibike.

Awali Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, (RUWASA) Mkoa wa Njombe, Mhandisi Sadick Chakka alisema miradi 99 ya maji imekamilika tangu mwaka 2020 hadi Disemba 2024 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 43.4

"Miradi hiyo imeweza kunufaisha wakazi zaidi ya 177,989 hii ni sawa na asilimia 20 ya wakazi wote 889,946 waliopo katika Mkoa wa Njombe," alisema Mhandisi Chakka.

Alisema mradi wa kitaifa wa miji 28 ambao umetengewa Sh. bilioni 205.93 kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maji itakayowawezesha wananchi wapatao 452,847 kwa miji ya Njombe, Wanging'ombe na Makambako kwa kupata maji ya uhakika na yenye kutosheleza.

"Hadi sasa utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 11 kwa ujumla ambapo kazi zilizoanzwa kutekelezwa ni ujenzi wa vyanzo, ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji na ujenzi wa matangi," alisema Mhandisi Chakka.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Makambako (MAKUWASA) Mhandisi Oscar Lufyagile alisema wanakabiliwa na tatizo la makandarasi wanaotekeleza mradi wa miji 28 kutotii maelekezo yao.




Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, katika viwanja vya Mwembetogwa, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Polisi yafunga vituo vitano mafunzo udereva

**Na Gideon Mwakanosya,**

SONGEA

KIKOSI cha Usalama Barabarani Mkoa wa Ruvuma kimevifunga vyuo vitano vya udereva vilivyopo Halmashauri ya Manispaa ya Songea baada ya kubaini kuwa havina sifa ya kutoa mafunzo.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Polisi Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana kuhusiana na kikosi hicho kuanza kufanya ukaguzi wa magari ili kudhibiti ajali za barabarani katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwaka huu wa 2024.

Chilya, alisema ukaguzi huo unafanywa na askari hao kwa magari ya vyuo vya mafunzo ya udereva, magari makubwa ya mizigo, abiria, mabasi yaendayo mikoani, wanafunzi na daladala ili kuhakikisha wasafiri na mali zao wanakuwa salama.

Akizungumzia kuhusu kufungwa kwa vyuo hivyo, alisema askari wa kikosi hicho walipofanya ukaguzi wa magari yanayotumika kutoa mafunzo, walibaini baadhi ni mabovu na kuamuru kufungwa kwa kukosa sifa ya kutoa mafunzo hayo.

Alisema vyuo hivyo vinamilikiwa na baadhi ya makanisa katika halmashauri hiyo.

Kuhusu mabasi ya kubeba wanafunzi, alisema wameamua kuyafanyia uchunguzi kutokana na shule nyingi kufungwa ili kubaini mabovu na kwamba zitakapofunguliwa yawe salama kusafirisha wanafunzi kwenda shuleni.

Kwa upande wa madereva, alisema watano wamefungiwa leseni zao baada ya kukutwa na makosa ya kukiuka sheria za usalama barabarani.

Alisema makosa hayo ni kuendesha gari kwa uzembe na kugonga gari nyingine kwa nyuma, kupita magari mengine bila kuchukua tahadhari kwa watumiaji wengine wa barabara, kuzidisha abiria na kumruhusu kondakta kuendesha gari la abiria bila kuwa na leseni.

"Jeshi la Polisi linaendelea kuwakumbusha madereva na wamiliki wa vyombo vya moto kuchukua tahahadhari katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka kwa kuwa kina matukio mengi ya ajali kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini," alisisitiza Kamanda Chilya.

Yasini Nungu, dereva wa mabasi yanayosafirisha wanafunzi mjini Songea, ameliomba jeshi hilo kuwadhibiti madereva bodaboda na magari kuwa makini kwenye maeneo ya vivuko vilivyowekwa barabarani.

Nungu pia ameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kuweka taa za barabarani ili kupunguza ajali.

## EWURA yakoshwa na miradikuzalisha umeme jotoardhi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BODI ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeridhishwa na hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme wa jotoardhi kwenye maeneo ya Ngozi (MW 70) na Kyejo-Mbaka (MW 60) mkoani Mbeya.

Ziara ya kutembelea miradi hiyo iliongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Mark Mwandosya imelenga kuona hatua iliyofikiwa katika uendelezaji wa miradi hiyo muhimu ya kimkakati.

Akizungumza jana baada ya kutembelea mradi huo , Prof. Mwandosya alisisitiza umuhimu wa kupanua wigo wa vyanzo vya kuzalisha umeme ikiwemo jotoardhi, ili kuboresha upatikanaji wa huduma za nishati kwa wananchi.

"Ni wakati sasa wa kuwekeza zaidi katika vyanzo vingine vya kuzalisha umeme, hususani jotoardhi, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu. Nishati ni injini ya maendeleo, na tuna kila sababu ya kutumia rasilimali tulizo nazo kwa ufanisi," alisema Prof. Mwandosya.

Aidha, Prof. Mwandosya aliipongeza Kampuni ya Maendeleo ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) kwa juhudi zake za kuhakikisha miradi hiyo inasonga mbele.

Alielezea kufurahishwa kwake na msukumo uliopo katika kuendeleza rasilimali watu kupitia mafunzo akisema kuwa juhudi hizo ni muhimu kwa ustawi wa sekta ya nishati nchini.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Umeme wa EWURA, Mhandisi Aurea Bigirwamungu, alisisitiza dhamira ya kushirikiana na wadau wote kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa mafanikio.





## Kilimo cha kakao kuanzishwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Misitu inatarajia kuanzisha kilimo cha kakao visiwani hapa kwa ajili ya kupata fedha za kigeni na kuongeza kipato kwa wakulima.

Mpango huo ulitangazwa jana na Ofisa Mkuu wa Kilimo wa Wizara hiyo, Salum Rehani Mwinyi, wakati akizungumza na mwandishi wa habari ofisini kwake Mwanakwareka visiwani hapa.

Mwinyi, alisema wizara hiyo inatarajia kuanzisha kilimo cha kakao kama zao mbadala la biashara ili kusaidiana na zao la karafuu.

Alisema mpango huo umekuja baada ya kubaini kuwa karafuu linakabiliwa na changamoto za uzalishaji hivyo ipo haja ya kuwa na mazao mbadala kama nchi yatakayosaidia kupata fedha za kigeni na kuinua maisha ya wananchi.

"Kilimo cha kakao kinaweza kusaidiana na karafuu kuimarisha uchumi kwa sababu nalo ni miongoni mwa mazao ya kitropiki ambalo kwa mazingira ya Zanzibar linaweza kustawi maeneo yote ya Unguja na Pemba," alisema Mwinyi.

Alisema mkulima anaweza kupanda kakao katika hali tofauti kwa kuchanganya na mazao ya minazi, parachichi, migomba, mbogamboga na mikarafuu na kupata mavuno ya kutosha na kipato.

Hata hivyo, Mwinyi, alisema kupitia kakao, mkulima anaweza kupata mavuno zaidi ya karafuu kwa mti kwa kipindi cha kati ya miaka sita hadi 10 kwa mbegu zilizofanyiwa utafiti.

"Utafiti uliofanywa na wataalamu kuhusiana na kokoa unaonyesha uzalishaji wa kokoa huanza miaka mitatu baada ya kupanda na ikifika mitano unaanza kufikia uzalishaji wa juu kwa kilo tano mpaka 10 za kokoa kavu tofauti na mti wa mkarafuu," alisema.

Mwinyi, alisema kwa Tanzania Bara uchunguzi wa kitaalamu umebaini wakulima wengi wamewekeza katika kakao hasa vijana na wanawake.

# Norway yaonesha matumaini kwa wanawake mwaka 2025

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Balozi wa Norway nchini, Kjetil Schie amesema mwongozo wa sera ya jinsia kwa vyama vya siasa utaongeza idadi ya wanawake kujitokeza kuwania uongozi wa majimbo nchini katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Schie, alitoa kauli hiyo jana visiwani hapa katika mkutano wa uzinduzi wa mwongozo wa sera ya jinsia na madawati ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia kwenye vyama hivyo.

Alisema Norway inafurahishwa na juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya mageuzi ya sheria hususani za kuhusu uchaguzi na kuweka mazingira mazuri kwa wanawake kushiriki kugombea kwenye majimbo nchini.

Schie, alisema kuwapo kwa sera hiyo kufungua milango kwa wanawake kuingia katika nafasi za uchaguzi majimboni, hivyo kufikia asilimia 50 kwa 50 ya uongozi wa kisiasa kati yao na wanaume.

Hata hivyo, alisema hadi sasa idadi ya wajumbe wanawake kwenye Baraza la Wawakilishi na wabunge kwenye majimbo hayo visiwani hapa katika vyombo vya maamuzi si nzuri, hivyo haitoi nafasi kwa jamii ya wanawake kusikika sauti zao.

"Sisi tunaamini ukimwezesha mwanamke unakuwa na jamii imara yenye uwezo wa kiuchumi na kuleta mageuzi muhimu ya maendeleo," alisema balozi huyo.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema kuna matumaini makubwa ifikapo mwakani wanawake wengi watajitokeza kushiriki uchaguzi huo baada ya kupata mafunzo ya kuwajengea uwezo kupitia Mradi wa SWILL.

Dk. Issa, alisema zaidi ya wanawake 900 wamejengewa uwezo kupitia mradi huo unaofadhiliwa na ubalozi huo kwa lengo la kuwawezesha kujitosa kwenye kinyang'anyiro hicho kitakachovishirikisha vyama vingi vya siasa visiwani hapa

"Tunatekeleza mradi wa kujenga uwezo wanawake kuingia katika harakati za kisiasa kupitia Mradi wa SWILL, matarajio yetu makubwa kuona katika uchaguzi mkuu wa mwakani idadi ya wanawake inaongezeka katika harakati za kisiasa," alisema.

Baadhi ya wanawake watia nia, wameahidi kuchukua fomu kuwania uongozi katika majimbo ya uchaguzi wakati utakapofika ili kuingia katika vyombo vya kutunga sheria.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, akimfariji Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, Mwaka Mrisho Abdalla (kushoto), anayesumbuliwa na matatizo ya kiafya, alipomtembelea nyumbani kwake, kijiji cha Ubago Wilaya ya Kati, juzi. Kulia ni Katibu wa chama hicho mkoa, Abdalla Mwinyi Hassan. **PICHA: IS-HAKA OMAR**

# Viongozi kikaangoni kwa kukiuka maadili ya kazi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imeiagiza Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuwachukulia hatua viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili na kukwamisha wananchi kupata maendeleo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, wakati akizungumzia Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu nchini.

Abdulla, alisema lengo la maadhimisho hao ni kuwaongezea uwelewa viongozi wa umma na wananchi kuhusu umuhimu wa maadili, utawala wa sheria, haki na usawa, uadilifu na uwajibikaji na kuzuia rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika maadhimisho hayo yaliyofanyika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete Pemba, alisema tume hiyo kwa kushirikiana na mamlaka nyingine, inapaswa kuwachukulia hatua viongozi hao na watumishi wa umma ili kudhibiti vitendo hivyo.

Awali, alisema kila taasisi inapaswa kutekeleza misingi ya utawala bora ili kuimarisha uadilifu, haki za binadamu na kuzuia rushwa ili serikali ifikie malengo ya kuwapatia maendeleo wananchi.

Abdulla, alisema taasisi zinazosimamia utawala bora ikiwamo tume hiyo na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora zimepiga hatua na kuendelea kupata mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema tume hizo zimedhibiti mianya ya rushwa, upotevu wa mapato ya serikali na kuhakikisha fedha zinazotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwezi zinazopelekwa kila wizara, idara na taasisi na kutumika kwa mujibu wa utaratibu.

Alisema kuongezeka kwa idadi ya hati safi za ukaguzi wa hesabu ni uthibitisho wa kuimarika uwajibikaji katika usimamizi na matumizi ya rasilimali za umma, huduma za afya, elimu, maji na miundombinu.

Abdulla, aliwataka viongozi hao kufanya kazi kwa kufuata sheria na miongozo ya kazi zao ili kufanikisha malengo ya serikali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema ni jukumu la viongozi na watumishi wa umma kuwa na uzalendo, uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika utendaji kazi.

Waziri Haroun, alisema wizara yake inatoa elimu kupitia vyombo vya habari ili kuhakikisha inawafikia viongozi, watumishi wa umma na wananchi.

Akiwasilisha mada juu ya umuhimu wa usimamizi wa rasilimali za umma na mapambano dhidi ya rushwa katika kuimarisha utawala bora, Jaji Ibrahim Mzee Ibrahim, alitaja makosa ya kisheria ambayo viongozi na watumishi wa umma wanatakiwa kujiepusha ni kutoa ni kupokea rushwa, usimamizi na matumizi mabaya ya rasilimali za umma na madaraka.

# Wakuu nchi jirani waja kuzindua kituo mauzo umeme TANESCO kimataifa

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema kuwa mwezi Februari mwakani itazindua mradi mkubwa wa maporomoko ya umeme wa Rusumo wenye megawati 80 katika kata ya Rusumo, Wilaya ya Ngara, unaotekelezwa kwa pamoja na nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko, alisema hayo mkoani Dodoma katika hafla ya kuweka jiwe la msingi mradi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka chalinze hadi Dodoma utakaogharimu Sh. bilioni 513.

Alisema mradi huo utakaozinduliwa na wakuu wa nchi kutoka nchi hizo, ni sehemu ya mipango ya serikali ya kuziunganisha na umeme na njia za kusafirishia umeme nchi inazopakana nazo.

Alisema kwa sasa imeshajiunganisha na nchi za Burundi, Rwanda, Kenya na sasa inaiunganisha Zambia na wanaelekea Malawi.

Lengo ni kuhakikisha kuwa umeme uliopo nchini unatumika kufanya biashara kwa kuwa kwa sasa nchi ina umeme mwingi kuliko mahitaji.

"Ni dhamira ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwamba kila aliye jirani yetu kupitia mpango wa Eastern African Power Pull na SADC power pull sisi tunakuwa na mchango mkubwa kuwapatia nishati jirani zetu," alisema.

Alimwelekeza mkandarasi anayesimamia mradi huo kuhakikisha kuwa unamalizika kwa wakati na ubora unaohitajika na kuwaagiza Meneja Mradi wa TANESCO pamoja na taasisi nyingine zinazosimamia mradi huo kuhakikisha kuwa wanasimamia utekelezaji wa mradi huo kama Rais Samia alivyoagiza.

Alisema lengo la nchi ni kuhakikisha umeme mwingi unafika Dodoma ili baadaye usafirishwe kupelekwa nchi jirani.

WIZI VIFAA

Biteko aliwakumbusha Watanzania kuwa ni jukumu lao kuilinda na kuitunza miundombinu ya umeme kwa kuwafichua wanaoihujumu kwa kuwa serikali inatumia gharama nyingi kuijenga ili iiletee nchi maendeleo.

"Sasa wapo wengine ambao wanahujumu tu miundombinu, mtu akipanda pale akakata waya ule, atawatoa watu wengi kwenye umeme, watu wengi hawatajua mwizi wao wanamjua TANESCO amekata umeme," alisema.

Alisema, Kisambule Mkoa wa Pwani, amekutwa Mtanzania ana shehena kubwa aliyohifadhi nyaya za umeme, na kuagiza vyombo vya dola kuhakikisha kuwa mtu huyo anachukuliwa hatua za kisheria ili iwe fundisho.

Waziri wa Nishati, Innocent Bashungwa, aliwahakikishia Watanzaia kuwa miundombinu ya umeme italindwa kwa nguvu kubwa na kutoa onyo kwa wahalifu wanaochezea miundombinu hiyo kuwa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi watawakamata watu hao na kuwafikisha kwenye sheria.

Alisema serikali kupitia kodi ya Watanzania inajenga miundombinu hiyo kwa gharama kubwa na haitomvumilia mtu yeyote atakayeiharibu.

Mkurugenzi wa Benki ya Dunia (WB), Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, Wendy Hughes, alipongeza serikali kwa hatua hiyo muhimu ambayo itaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi ikiwamo upatikanaji wa umeme wa uhakika na nafuu.

Alisema Benki ya Dunia inalenga kuwafikia zaidi ya milioni tatu barani Afrika ifikapo mwaka 2030 kwa kuwasambazia umeme na imetenga kiasi kikubwa cha fedha kufikia malengo hayo.

Alimhakikishia Naibu Waziri Mkuu kuwa wabia wote wa maendeleo wapo tayari kuiunga mkono Tanzania kuhakikisha kuwa malengo ya maendeleo yote waliojiwekea yanatimia.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO, Dk. Rhimo Nyansaho, alisema mradi huo ni muhimu kwa shirika hilo kwa kuwa kupitia kuunganishwa na njia za umeme na nchi itaweza kuuza umeme kwa nchi jirani na watanufaika kwa kuongeza mapato na kutokutegemea ruzuku ya serikali.

Alisema kuwa mradi huo ni muhimu kwa sababu upatikanaji wa umeme wa uhakika unachochea maendeleo ya viwanda hivyo kuwa na uhakika wa bidhaa.

Alisema pia mradi huo unakwenda kuongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati na kuvutia wawekezaji kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza nchini na kuiongezea nchi mapato.

Aidha, mradi huo ni muhimu kwa TANESCO kwa kuwa utaongeza mapato na taasisi hiyo kupitia kuuza umeme nje ya nchi hivyo kuondokana na utegemezi wa ruzuku za serikali.

Alisema bodi hiyo itahakikisha kuwa mradi huo unakamilika kwa wakati na kwa ubora uliotegemewa.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Mhandisi Gisima Nyamhanga, alisema kuwa mradi huo sehemu ya mfumo wa maendeleo ya mfumo wa gridi ya taifa yaliyobainishwa katika mpango kabambe wa mwaka 2020.

Alisema mpango huo una lengo la kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika ili kuwezesha ukuaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi na usalama wa nishati ya umeme nchini na ukanda wa Afrika Mashariki.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms/WhatsApp: +255 677 020 701***
***Email: costomerrelations@guardian.co.tz***

## TCRA yataka waandaaji maudhui kuzingatia maadili, Kiswahili sanifu

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewataka watayarishaji wa filamu nchini kuzingatia viwango vya ubora na kudumisha maadili ya kitamaduni ya taifa, ikiwa ni pamoja na kukuza Kiswahili sanifu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri K. Bakari, alisema katika ujumbe wake kwa wadau wa tasnia ya filamu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kuwa, wazalishaji wa filamu wana wajibu wa kutangaza maudhui yanayozalishwa ndani ya nchi.

Ofisa Mawasiliano Mkuu wa Mamlaka TCRA, Semu Mwakyanjala, akiwasilisha mada kwenye mkutano wa wadau wa tasnia ya filamu, alisema ni muhimu wakatambua kuwa maudhui yao ina nafasi kubwa ya kuathiri jamii moja kwa moja katika kujenga mitazamo ya watu.

"Uzalishaji wa filamu lazima usikose viashiria vya athari chanya. Filamu zinapaswa kubadilisha na kuboresha viwango vya maisha huku zikidumisha umoja na maelewano ya kitaifa," alisema.

Aidha, alibainisha kuwa tasnia ya filamu ndio chanzo kikuu cha utangazaji wa ndani.

"Kanuni zinahitaji redio na televisheni za Tanzania kuhakikisha zinatangaza angalau asilimia 60 ya maudhui ya ndani. Filamu lazima ziwe na umuhimu kwenye jamii. Hazipaswi kupingana na tamaduni, imani na kanuni za watu," aliongeza.


"Uzalishaji wa filamu pia unapaswa kuzingatia kukuza maadili ya kitaifa na tunu za kipekee zinazotambulisha nchi. Hii ni msingi thabiti ambayo Jumuiya ya Watanzania imeanzishwa," alisema.

Alitoa wito kwa wahusika wa TFFA kuzingatia sheria kanuni na taratibu za utengenezaji wa filamu na wanapaswa kutumia lugha inayokubalika katika jamii.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Dk. Genad Kasiga, alisema tasnia ya filamu ni miongoni mwa sekta zinazozalisha kipato na ajira. Pia ilikuwa ni jukwaa la kukuza vipaji.


Alisema TCRA inasimamia maudhui ya utangazaji na inayo Kamati ya maudhui ya watu watano, na kwamba kamati inafuatilia na kusimamia maadili ya utangazaji.

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**EMMANUEL FELIX MBUYA** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TAE240143** iliyotolewa uhamiaji makao makuu tarehe 14 /11/2019. Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi:**PHQ/DAR/KIN/267691/2024**

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HAPPY ELIAKIM MWANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TAE181578** ILIYOTOLEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUPITIA MAMLAKA YA UHAMIAJI YA NCHI HIVYO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA HATI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/MOR/MOR/42819/2024.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**MUSO KAROJE** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Stashahada ya Ualimu wa Sekondari cha Chuo cha Ualimu Butimba chenye Index namba **E 0501-0197** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania Mwaka 2008. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KBR/RB/215/2012**

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai / Ndoa Na. 1723/2024**

**Jina la Mdai: PASCAL ANDREW MAYALLA**

**Jina la Mdaiwa: JOYCE ABEL MMARI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: JOYCE ABEL MMARI**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba TALAKA – KUSIKILIZWA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 12 mwezi 12 mwaka 2024 saa 8:30 mchana mbele ya Mh. MWAGENI kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama leo tarehe 3 mwezi 12 mwaka 2024.

HAKIMU

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **WEMA SHAHA KASEBA** amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 962CTG** aina ya **TOYOTA PORTE** chassis namba **NNP110025027,** engine **1NZB578605.** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/261385/2024**

HABARIKIMATAIFA

# Al Bashir amrithi Assad Syria, Iran, Marekani zashutumiana

**DAMASCUS, Syria**

SIKU chache baada ya kupinduliwa kwa Rais Bashar Al Assad, Syria imeanza kupiga hatua mpya baada ya kiongozi wa waasi, Mohammed Al-Bashir, kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa serikali ya mpito.

Al-Bashir ambaye ni mkuu wa zamani wa utawala wa waasi katika eneo la kaskazini-magharibi mwa nchi hiyo, aliwataka raia wa Syria kuwa watulivu na kuwa wamoja katika kipindi hicho cha mpito.

Waziri mkuu huyo amepewa jukumu la kuongoza serikali hadi Machi 2025.

Bashir kwa mara ya kwanza aliongoza mkutano uliohudhuriwa na wajumbe wa serikali yake mpya na wale wa baraza la mawaziri la zamani la Assad kujadili makabidhiano ya nyadhifa na taasisi.

Huku kukiwa na dalili za kurejea kwa maisha ya kawaida katika mji mkuu wa Syria wa Damascus, raia bado wanapata shida kuondokana na hali ya woga iliyotokana na utawala wa rais wa zamani Bashar al-Assad.

Katika jiji la Damascus, maduka mengi na migahawa imefunguliwa, lakini vituo vya mafuta ambavyo vyote vinamilikiwa na serikali, bado havijafunguliwa.

Baadhi ya familia walikuwa wakipeana peremende katika kusherehekea serikali mpya ambayo imeanza kazi.

"Sasa tunaweza kuzungumza kwa sauti kubwa, bila uoga," kijana mmoja aliambia BBC huku akitabasamu.

Mwanamke mwingine alisema „Ni kana kwamba tunaweza kupumua kwa urahisi zaidi sasa."

Hata hivyo, Marekani ilisema itaiunga mkono serikali mpya endapo itatokana na mchakato unaoaminika, unaojumuisha watu wote na unaoheshimu jamii ya walio wachache.

Iran yaishutumu Marekani

Kiongozi wa juu wa Iran, Ayatullah Ali Khamenei, amesema kuanguka kwa Rais Bashar al-Assad, kulipangwa kwenye vyumba vya mikakati vya Marekani na Israel.

Ayatullah Khamenei, ambaye ndiye mwenye nguvu kubwa kisiasa nchini Iran, alisema jana kuwa nchi yake ina ushahidi unaothibitisha kwamba kupinduliwa kwa Rais Assad ulikuwa mpango wa Israel, Marekani na jirani mmoja wa Syria, ambaye hakumtaja.

Hata hivyo, wachambuzi wanasema nchi hiyo huenda ikawa ni Uturuki, ambayo imekuwa ikipambana na wale inaowaita magaidi kwenye mpaka wake na Syria kwa miaka mingi.



Watu wakitembea karibu na sanamu katika jiji la Damascus, baada ya waasi wa Syria kumwondoa madarakani Rais Bashar al-Assad, nchini humo. **PICHA: REUTERS**

Iran, ambayo ilikuwa mshirika mkubwa wa utawala wa Assad, inatajwa kuwa mmoja wapo wa waathirika wakubwa wa kuporomoshwa kwa utawala huo, hasa kupitia kile kiitwacho Muungano wa Mapambano, ambao unaongozwa na taifa hilo la Ghuba ya Uajemi na ukizijumuisha Yemen, Syria, makundi ya Hizbullah nchini Lebanon na Hamas katika Ukanda wa Gaza.

„Anayedhani kuwa kudhoofika kwa muungano wa mapambano kutaidhoofisha Iran, atakuwa hajajuwa kabisa maana ya mapambano." Alisema kiongozi huyo wa Iran.

**MAREKANI, UTURUKI KUKUTANA**

Kwa upande mwengine, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken, anatazamiwa kuwasili nchini Uturuki kukutana na waziri mwenzake, Hakan Fidan, Ijumaa ya wiki hii.

Chanzo kimoja kutoka Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Uturuki kilisema jana kuwa lengo la ziara ya Blinken ni kuzungumzia hali ya Syria baada ya kupinduliwa kwa Assad.

Chanzo hicho hakikueleza undani wa mazungumzo kati ya pande hizo mbili, lakini kauli za awali kutoka utawala unaomaliza muda wake wa Rais Joe Biden, unasisitiza kuhakikisha utawala mpya wa Syria hautakuwa na mafungamano wa maadui wa Marekani na Israel kwenye eneo hilo la Mashariki ya Kati.

**ISRAEL YAISHAMBULIA SYRIA**

Katika hatua nyingine, Israel imethibitisha kufanya mashambulizi ya anga dhidi ya vituo vya kijeshi vya Syria, bandari na maeneo nyeti ambavyo wanajeshi wake walikimbia kufuatia kupinduliwa kwa serikali.

Jeshi la Israel lilisema limeshambulia maghala ya kimkakati ya silaha ndani ya saa 48 zilizopita.

Waziri wa Ulinzi, Israel Katz, alisema mashambulizi yao yanadhamiria kuanzisha eneo la kujilinda kusini mwa Syria ambalo litasimamiwa bila kuwapo wanajeshi wa kudumu.

Aidha, Israel ilithibitisha kushambulia meli za kivita za Syria, ikiwa ni sehemu ya juhudi zake za kuondosha vifaa vya kijeshi nchini humo baada ya kuanguka kwa utawala wa Assad.

Katika taarifa yake jeshi la ulinzi la Israel (IDF) ilisema meli zake zilishambulia bandari za Al-Bayda na Latakia Jumatatu usiku, na kuziharibu meli 15 zinazotia nanga.

BBC imethibitisha video zinazoonyesha milipuko katika Bandari ya Latakia, zikionyesha uharibifu mkubwa kwa meli na sehemu za bandari.

IDF pia ilisema ndege zake za kivita zimefanya mashambulizi zaidi ya 350 ya anga katika maeneo mbalimbali ya Syria, wakati yakihamishia vikosi vya ardhini katika eneo la mpakani kati ya Syria na milima ya Golan inayokaliwa na Israel.

Shirika la Uangalizi wa Haki za Binadamu la Syria lenye makao yake nchini Uingereza (SOHR), lilisema kuwa limerekodi zaidi ya mashambulizi 310 yaliyofanywa na Israel tangu serikali ya Syria ilipopinduliwa na waasi siku ya Jumapili.

**VERDI YAONYA WASYRIA**

Wakati hayo yakiendelea, umoja wa vyama vya wafanyakazi nchini Ujerumani (Verdi), umeonya dhidi ya hatua ya kuwarejesha nyumbani maelfu ya Wasyria waliopewa hifadhi kufuatia kupinduliwa kwa Bashar al-Assad.

Kupitia mahojiano yake na Shirika la Habari la Ujerumani (DPA), mkuu wa umoja huo, Frank Werneke, alisema kwamba kuwafukuza Wasyria ni kinyume na maslahi yao na pia kinyume na maslahi ya soko la ajira ndani ya Ujerumani yenyewe.

Badala yake, mkuu huyo wa wafanyakazi aliitaka serikali ya Ujerumani na za Umoja wa Ulaya kwa ujumla kuchukuwa tahadhari kutokana na kile kinachoonekana kuwa ni wimbi la hatua mbaya dhidi ya wahamiaji kutoka Syria.

***Vyanzo: BBC, DW***

# MWENDA AANZA MAZOEZI YANGA

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja tu baada ya kutangazwa rasmi kujiunga na Yanga kwa mkopo akitokea Singida Black Stars, beki wa pembeni Israel Mwenda tayari ameanza mazoezi na timu hiyo.

Tetesi za Yanga kutaka kumsajili beki huyo wa zamani wa Simba zilianza kusikika juzi na jana asubuhi kupitia kurasa zao za mitandao ya kijamii walitangaza kumsajili beki huyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa klabu hiyo, Ally Kamwe alisema mchezaji huyo hakutaka kuchelewa baada yakusaini mkataba jana asubuhi alishiriki mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika uwanja wa KMC.

"Kijana hajataka kuchelewa leo asubuhi (jana) ameungana na wenzake kufanya mazoezi ya pamoja chini ya kocha Saed Ramovic," alisema Kamwe.

Mwenda amejiunga na Yanga kwa mkopo akitokea Singida Black Stars timu aliyojiunga nayo kwenye dirisha kubwa la usajili akitokea Simba.

Usajili wake kwenda Singida Black stars ulileta sintofahamu kutokana na awali kuelezwa alikuwa ameshasaini mkataba mpya na Simba hali iliyopelekea kurejesha fedha kwa ajili waker hao kabla ya kusaini mkataba na walima alizeti hao.

Inaelezwa beki huyo anaenda kuchukua nafasi ya Shadrack Boka raia wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambaye ni majeruhi na bado haifahamiki atarejea lini uwanjani kutokana na kuuguza majeraha yake.




Mchezaji mpya wa Yanga, Israel Mwenda akiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kwa mara ya kwanza jana kwenye Uwanja wa KMC. **PICHA: YANGA**

## Uhamiaji yaipania Malindi FC

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KLABU ya Uhamiaji leo inashuka uwanjani kucheza na Malindi Fc kwenye mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar huku wakipania kuondoka na pointi tatu ili ziwapandishe juu kwenye msimamo.

Kwa sasa Uhamiaji FC inashika nafasi ya tisa kwenye msimamo ikiwa na pointi 20 wakati wapinzani wao Malindi SC wapo nafasi ya sita wakiwa na pointi 23.

Mchezo huo w aleo utakaochezwa uwanja wa Mau utakuwa wa kukamilisha mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo Abdisalehe Abdallah, alisema wanashuka uwanjani kwenda kuchukua alama tatu katika mchezo huo ambao ameutabiri kuwa mgumu.

Alisema benchi la ufundi wameiandaa timu hiyo vizuri na watacheza kwa mipango ili kufanikisha kupata ushindi katika mchezo huo muhimu.

Alisema anatambua utakuwa mchezo mgumu kutokana na matokeo waliyopata wapinzani wao katika mchezo wao uliopita ambao walipoteza.

Alisema katika mchezo wa leo atаingia na mbinu mbadala ili kuona wanafuta makosa yao na kupata matokeo ya ushindi.

"Mchezo utakuwa mgumu, lakini tumejiandaa kuhakikisha tunawakabili wapinzani wetu, hatupo nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi hivyo tunahitaji point tatu muhimu ili tumalize mzunguko tukiwa nafasi nzuri na kujiandaa kuelekea mzunguko wa pili"alisema.

Aidha alisema wanashuka uwanjani wakiwa tayari wameshazisoma mbinu za wapinzani wao katika mchezo wao wa mwisho walicheza.

# Wakongwe kuiimarisha Pamba Jiji FC

**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Simba, Habib Kyombo anatarajiwa kujiunga na klabu ya Pamba Jiji FC kwa mkopo akitoka Singida Black Stars, huku pia wakitajwa wakongwe wengine Kelvin Yondani na Deus Kaseke kuwa njiani kujiunga na timu hiyo.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema mazungumzo ya pande zote yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika wakati wowote kabla ya kutangazwa kuwa wachezaji wa timu hiyo.

Imeelezwa kuwa Singida Black Stars imekubali kumtoa Kyombo kutokana na kutokuwa na nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza hivyo kuamua kumtoa ili apate muda wa kucheza.

"Singida wanaona akija Pamba Jiji FC atapata muda mrefu wa kucheza kwa sababu wao wamejitosheleza na wana mastraika hadi wakigeni, lakini sisi tunamhitaji aje kusaidiana na George Mpole," kilisema chanzo hicho cha taarifa hiyo nadani ya Pamba Jiji FC.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Biko Kotecha, amekiri kuwa ni kweli wanatarajia kufanya usajili kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi, lakini alikataa kutaja majina ya wachezaji watakaowachukua.

"Usajili mdogo tumejipanga vizuri, tunataka kuziba mapengo yaliyoonekana kutugharimu mechi nyingi za mzunguko wa kwanza, muda utakapofika tutawaambia ni nani na nani kwa sasa itoshe tu kuwaambia kuwa tuko kwenye harakati ya kupata wachezaji bora na kuwaingiza ndani ya kikosi chetu. Kwa sasa tuache taratibu za machakato wa usajili uendelee kwanza," alisema mwenyekiti huyo.

Mchezaji huyo alijiunga na Simba 2022, akicheza kwa msimu mmoja kabla ya kwenda kujiunga na Singida Black Stars.

Mbali na straika huyo, habari zinasema Pamba Jiji imewasajili pia wachezaji wa zamani wa Yanga, Yondani na Kaseke kwa ajili ya kukiimarisha kikosi.

Timu hiyo inayoshika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 11, jana ilitarajiwa kucheza mchezo wa ligi dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamhuyo, Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMPIGA BEI RASHFORD
KLABU ya Manchester United inataka kumuuza mshambuliaji wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27 katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Sky Sport Germany)***

### ....YUMO NA MARTINEZ
UNITED pia inaweza kumuuza nyota wake Lisandro Martinez ikiwa Real Madrid itaongeza nia yao ya kumnunua beki huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 26. ***(Talksport)***

### ARSENAL YAMWINDA VLAHOVIC
ARSENAL inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Serbia mwenye umri wa miaka 24, Dusan Vlahovic kutoka Juventus Januari. ***(TeamTalk)***

### DIJK KUSAINI MKATABA LIVERPOOL
MLINZI wa kati wa Uholanzi, Virgil van Dijk yuko tayari kusaini mkataba mpya na Liverpool licha ya kukataa ofa ya awali. ***(Football Insider)***

### NEWCASTLE YAMFUATILIA BAKAYOKO
KLABU ya Newcastle United inamfuatilia winga wa PSV Eindhoven na Ubelgiji, Johan Bakayoko mwenye umri wa miaka 21, kabla ya dirisha la uhamisho la Januari. ***(Telegraph)***

### DAN ASHWORTH ATAKIWA ARSENAL
ARSENAL ina nia ya kumsajili Dan Ashworth kama Mkurugenzi wao mpya wa michezo baada ya kuondoka Manchester United. ***(ESPN)***

### SALAH KIMEELEWEKA LIVERPOOL
MAZUNGUMZO ya Liverpool kuhusu mkataba mpya na mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32 yanaendelea huku pande hizo mbili zikikaribia kuafikiana kuhusu muundo mpya wa malipo. ***(Sky Sports)***


### HERNANDEZ KURUHUSIWA MILAN
AC Milan iko tayari kumruhusu nahodha Theo Hernandez kuondoka katika klabu hiyo lakini itadai ada ya takribani pauni milioni 41 kwa beki huyo wa kushoto wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27. ***(Calciomercato)***

### ADARABIOYO KUBAKIZWA CHELSEA
CHELSEA haitafikiria kumruhusu mlinzi wa kati, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 27 kuondoka kwa mkopo Januari huku kukiwa na taarifa za yeye kutaka kuelekea West Ham. ***(Football Insider)***

### ERIKSEN KUONDOKA MAN UNITED
KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32, anatarajiwa kuondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### BARRY KUTOLEWA TENA KWA MKOPO
KLABU ya Aston Villa inafikiria kumwita Louie Barry mwenye umri wa miaka 21, kutoka kwenye mkopo kule Stockport County ili kumpeleka mshambuliaji huyo wa England mwenye mabao 14 kwa klabu iliyo katika kiwango cha juu zaidi. ***(TeamTalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ENRIQUE: PSG BADO IPO HATARINI UEF

Kauli hiyo ameitoa juzi licha ya ushindi walioupata akiweka wazi kuwa....

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa PSG, Luis Enrique alisifu timu yake baada ya ushindi wao wa mabao 3-0 dhidi ya RB Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini akasema lazima waimarike ikiwa wanataka kubakia kwenye kinyang'anyiro hicho.

Vinara hao wa Ligue 1 walivumilia mwanzo mbaya wa kampeni zao za Ligi ya Mabingwa msimu huu, kwa kufungwa na Atletico Madrid, Bayern Munich na washindi wa pili wa Ligi Kuu ya England msimu uliopita Arsenal.

Hata hivyo, ushindi wa Jumanne uliwaweka kwenye nafasi ya mchujo na sasa inashika nafasi ya 24 kwenye msimamo ikiwa na pointi saba kutokana na michezo sita.

Hata hivyo, kocha huyo alisema hiyo haitoshi.

"Soka ni mchezo wa matokeo bado tuna michezo miwili muhimu mbele, lakini bado tunaweza kuwa nje ya michuano," alisema kocha huyo.

"Huu haukuwa mchezo mzuri kuliko PSV Eindhoven au dhidi ya Atletico Madrid, naweza kusema hata ulikuwa mbaya zaidi, lakini hiyo ndio soka, tunajua tunatakiwa kuimarika na kikosi hakijabadilika sana.

Tunahitaji pointi, na tutajaribu kushinda mechi zinazofuata."

Kocha huyo, alisifu juhudi za Nuno Mendes, ambaye alifunga bao lao la pili.

"Nuno analeta suluhu nyingine kwa sifa zake za kimwili na kiufundi. Anaweza kukamilisha na kucheza mbele. Anacheza juu zaidi kwa sasa. Analeta mambo mengi. Lakini hilo linaweza kubadilika," alisema kocha huyo.

Enrique sasa ataelekeza mawazo yake katika michuano hiyo kwenye mechi dhidi ya Manchester City ya Pep Guardiola Januari 22, kabla ya kufunga kampeni yao dhidi ya VfB Stuttgart siku saba baadaye.

# Slot hajaridhishwa kiwango Liverpool

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot amesema anataka zaidi kutoka kwa timu yake baada ya ushindi wa 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kubainisha kuwa "sijafurahishwa" na uchezaji.

Liverpool walionekana kuwa bora zaidi kwenye uwanja wa Montilivi, lakini walipata ushindi huo kutokana na mkwaju wa penalti wa Mohamed Salah katika kipindi cha pili baada ya Donny van de Beek kumchezea vibaya Luis Díaz ndani ya eneo la hatari.

Ushindi huo unamaanisha kuwa Liverpool wanaendeleza rekodi yao nzuri barani Ulaya, baada ya kushinda mechi zote sita za Ligi ya Mabingwa msimu huu, lakini Slot alisisitiza kwamba kiwango chao lazima kiboreshwe ikiwa timu yake ina malengo ya kubeba taji hilo.

Akizungumza na TNT Sports baada ya mchezo huo, bosi huyo wa Liverpool alisema: "Ukiniuliza kuhusu mechi zote sita, nimefurahishwa na matokeo yote na matokeo katika mechi tano.

"Sijafurahishwa na matokeo ya usiku wa leo (juzi). Hasa mambo mawili. Ukicheza dhidi ya timu ambayo ina mawazo mazuri kuhusu soka, inajua jinsi ya kuleta mpira nje kama timu ambazo tumecheza hivi karibuni huko Real Madrid na Manchester City, unahitaji kuwa mkali sana.

"Lakini ikiwa unasubiri kushinikiza utatolewa kwa urahisi, timu hii inaweza kukusababishia matatizo.

"Ninawaonea huruma kwa sababu wanastahili zaidi ya pointi tatu. Tuna kipa wa aina yake.

Tulipopoteza mpira hatukuwa wakali vya kutosha. Hatukuwa na udhibiti wowote katika mchezo. Labda kipindi cha pili kilikuwa bora zaidi."

Moja ya faida kubwa kwa Liverpool ni kurejea kwa Alisson kwenye kikosi cha kwanza baada ya kukosekana tangu Oktoba 5 kutokana na jeraha la misuli ya paja.

# Mourinho: Sijasema Man City ishushwe daraja

**TURIN, Italia**



JOSE Mourinho amejibu madai ya Pep Guardiola kwamba yeye anataka kuona Manchester City inashushwa daraja kutoka Ligi Kuu kwa kusema anataka tu "haki katika soka."

Kocha huyo wa Fenerbahce, Mourinho, ambaye alianzisha upinzani mkali na kocha wa wakati huo wa Barcelona Guardiola wakati akiinoa Real Madrid kati ya 2010 na 2013, hivi karibuni alisema Guardiola ameshinda mataji matatu pekee ya Ligi Kuu England kwa haki.

Mourinho alisema hivyo baada ya Guardiola kuwajibu mashabiki wa Liverpool waliokuwa wakimzomea kwa kuwaonesha vidole sita ikiwa ni kuashiria mataji sita aliyoshinda akiwa Etihad.

Guardiola kisha akasema kwamba maoni ya Mourinho yalitokana na kuinonea wivu Man City.

Lakini akizungumza kabla ya mechi ya Fenerbahce ya Europa League dhidi ya Athletic Bilbao jana, kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Mourinho alisema kwamba maoni yake yametolewa kwa sababu anataka kuona haki.

"Sio kweli kwamba ninataka Man City ishushwe daraja," alisema Mourinho.

"Ni kweli kwamba napenda haki, na mara nyingi klabu ndogo zinaadhibiwa kwa kuongeza tu euro 5 au 10 kwenye bajeti ya usajili kutokana na sheria za haki ya usawa a usajili.

"Kwa mfano, niliteseka kule Roma kwa miaka mitatu na mapungufu makubwa juu yake. Sidhani ni sawa kwamba papa wakubwa, ninaposema papa, nasema papa wa kifedha huwa wanatafuta njia ya kuepuka sheria.

"Mimi ni mtu wa mpira wa miguu, mtu anayependa soka, zaidi ya kuwa mwanasoka wa kulipwa nina shauku kubwa, napenda haki katika soka. Lakini mbali na hayo, hakuna hisia mbaya," alisema Mourinho.



# MBAPPÉ APIGA BAO LA 50 UEFA

**ROME, Italia**

KYLIAN Mbappé alifunga bao lake la 50 kwenye maisha yake ya soka kwenye michuano ya Ligi ya mabingwa Ulaya Jumanne, lakini alitolewa nje baada ya kuumia kipindi cha kwanza wakati Real Madrid ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Atalanta.

Fowadi huyo wa kimataifa wa Ufaransa alitolewa dakika ya 35 baada ya kupata jeraha na Rodrygo alichukua nafasi yake.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba Mbappé aliumia misuli ya paja lake la kushoto na jana Jumatano alitarajiwa kufanyiwa vipimo.

"Mbappé ameumia kwenye paja lake," alisema Ancelotti akiiambia Movistar baada ya mechi.

"Itabidi tusubiri kuona, lakini sijui ameumia kwa kiasi gani. Hakuweza kukimbia. Ilikuwa inamsumbua, ikabidi tumbadilishe.

Madrid walipata ushindi wa 3-2 baada ya mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Vinícius Júnior na Jude Bellingham.

Hadi alipoondoka, ulikuwa usiku mzuri sana kwa Mbappé.

Alitumia sehemu ya ustadi ya kudhibiti kwa mguu wake wa kushoto pasi kutoka kwa Brahim Díaz kabla ya kumpita mlinzi haraka na kuachia shuti kwa mguu wake wa kulia na kujaa wavuni dakika ya 10.

"Nilimkumbatia, lakini sijui kuhusu jeraha lake. Tunatumai si kubwa sana," alisema Díaz akiiambia Movistar.

Bao hilo lilimaanisha Mbappé amefikisha mabao 50 katika mechi 79 na anashika nafasi ya nne kwa kufikisha idadi hiyo ya mabao kwa mechi chache zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa baada ya Ruud van Nistelrooy (mechi 62), Lionel Messi (66), na Robert Lewandowski (77).

Cristiano Ronaldo anaongoza orodha ya wafungaji wa muda wote wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabao 140, na Messi anafuata akiwa na 129.

Ushindi dhidi ya Atalanta ulikuwa ni wa tatu kwa Madrid katika awamu ya ligi iliyoboreshwa na kumwacha bingwa huyo mara 15 katika nafasi ya 18 kwenye msimamo.

"Ushindi muhimu, pamoja na pointi tatu na kwa ari, kuelekea Krismasi. Tunawarudisha wachezaji, Vini alicheza leo, Rodrygo alicheza, tutamrejesha Camavinga. Lazima tusubiri hadi Krismasi," alisema Ancelotti.

"Tunaweza kuingia katika nane bora kwenye msimamo wa Ligi ya Mabingwa. Lengo liko wazi, tuna michezo miwili, na lazima tushinde yote."

HABARI MICHEZO

# TANZANIA WASICHANA U-15 YAWEKA MGUU MMOJA CAF

**Na Mwandishi Wetu, KAMPALA**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya Tanzania ya umri chini ya miaka 15 imelazimishwa sare ya bila kufungana na wenyeji Uganda katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Afrika (CAF U-15) katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa St. Mary's Kitende jana.

Matokeo hayo yanaifanya Tanzania kufikisha pointi nne sawa na Uganda lakini inaongoza katika msimamo kutokana na kuwa na idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

Tanzania inahitaji ushindi wa aina yoyote katika mchezo wake wa mwisho dhidi ya Burundi utakaochezwa leo.

Katika mechi ya mapema asubuhi yosso wa Burundi wamepata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Rwanda.

Burundi sasa imefikisha pointi tatu na kukaa katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa michuano hiyo inayotarajiwa kumalizika leo.

Uganda yenyewe itamaliza michuano hii leo kwa kuwakaribisha Rwanda ambao wamepoteza mechi zao zote walizocheza.

Kwa upande wa wavulana, Tanzania imetoka sare ya bila kufungana dhidi ya wenyeji Uganda.

Sare hiyo inawafanya yosso hao wa Tanzania kufikisha pointi tatu na watamaliza michuano hiyo leo kwa kuvaana na Burundi wakati Somalia itapambana na Rwanda.




Mchezaji wa Simba Queens, Precious Christopher, akijaribu kuwatoka wachezaji wa JKT Queens, katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake uliochezwa Uwanja wa KMC Complex Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Singida BS kuibomoa Tabora United

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kabla ya kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili, klabu ya Singida Black Stars inatajwa kutaka kuwarejesha wachezaji wake wawili ambao wamekuwa wakifanya vizuri kwenye kikosi cha Tabora United wanapocheza kwa mkopo.

Wachezaji hao ambao wanatarajia kurejea Singida Black Stars ni Mourice Chukwu na Faria Odongo ambao wamekuwa muhimili wa Tabora United kwenye michezo ya Ligi Kuu.

Habari kutoka ndani ya Singida Black Stars, imesema imeamua kuwachukua wachezaji hao, kiungo mshambuliaji Chukwu raia wa Nigeria na beki wa kati raia wa Congo Brazaville, Odongo kuwarudisha nyumbani kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Jumapili ijayo.

Hata hivyo, kuna taarifa tofauti ndani ya klabu hiyo, zikisema uamuzi huo umekuja ili kukiimarisha kikosi cha Singida Black Stars.

Kama wachezaji hao watarejea Singida Black Stars ni wazi watakuwa wameidhoofisha Tabora United.

Tabora United inashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 21 huku Singida Black Stars ikiwa nafasi ya nne na pointi zao 24.

Hata hivyo, Singida Black Stars wana mchezo mmoja zaidi ya Tabora United waliocheza michezo 13 mpaka sasa.



# Simba yamtaka Rupia wa Singida BS

INATOKA UK. 24

saidia sana," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo.

Rupia, kwa sasa anakamata nafasi ya pili kwa ufungaji wa mabao Ligi Kuu, akiwa na mabao matano sawa na kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua huku wote wakiongozwa na straika Selemani Mwalimu wa Fountain Gate mwenye mabao sita.

Hata hivyo, wakati Simba ikianzisha mazungumzo hayo, imetajwa klabu ya Yanga nayo huenda ikapiga hodi Singida Black Stars kumtaka mchezaji huyo ili kwenda kuwa mbadala wa wachezaji Prince Dube na Jean Baleke.

Inasemekana kama Yanga itaingia kikamilifu kumtaka Rupia inaweza kufanikiwa kumpata kirahisi tofauti na Simba kutokana na ukaribu na viongozi wa pande hizo mbili.

Inadaiwa kuwa hilo ndilo linalowatia hofu baadhi ya viongozi wa Simba na kusisitiza asajiliwe Lukumbi raia wa Uganda badala ya Rupia ambaye watani zao pia wanamtaka.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema kutakuwa na maboresho madogo kipindi cha dirisha dogo la usajili kwa kuongeza baadhi ya wachezaji huku Elie Mpanzu akisubiria dirisha lifunguliwe tu aingizwe kwenye mfumo wa usajili.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, kwa upande wake naye amekiri kuwapo kwa mahoshero kwenye kikosi chake, lakini akitaka watakaosajiliwa kuwa ni wale watakaoingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza.

"Nataka watakaosaidia waingie moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza, siyo wa kujaza nafasi au kusubiri wenzao kwanza, na kama wakikaa nje, basi ni kwa sababu ya ushindani wa namba siyo kiwango," alisema kocha huyo.

# Michezo

Alhamisi Desemba 12, 2024

Nipashe


**Mbappé apiga bao la 50 UEFA**

UKURASA 22



# SIMBA SC YAMTAKA RUPIA WA SINGIDA BS

●●●Yanga nayo yatajwa kuulizia uwezekano wa kumsajili ili...

**Na Adam Fungamwanngo**

KLABU ya Simba imeanza mazungumzo na Singida Black Stars kuangalia uwezekano wa kumsajili straika hatari wa timu hiyo raia wa Kenya, Elvis Rupia, kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa na Leonel Ateba na Steven Mukwala.

Taarifa za ndani zinasema wakati Simba wakianzisha mazungumzo hayo, watani zao, Yanga nao wanataka kutupa karata yao ya kumsajili mshambuliaji huyo ilikwenda kuongeza nguvu eneo lao la ushambuliaji.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema viongozi wa Simba wamegawanyika sehemu mbili, wengine wakimtaka straika wa kimataifa wa Uganda, Denis Lukumbi anayeichezea klabu ya Kitara FC ya Ligi Kuu nchini Uganda, lakini wengine wakimtaka Rupia katika kipindi cha usajili cha dirisha dogo kinachotarajiwa kufunguliwa Jumapili ijayo.

Wanaomtaka straika huyo wa Singida Black Stars wametoa sababu kuwa tayari ameizoea ligi ya Tanzania na mikiki yake, hivyo hakutakuwa na mambo ya kumpa mtu muda.

"Wengi wanamtaka Rupia, pamoja na umahiri wake wa kupachika mabao, lakini hakutakuwa na mambo ya kumpa mtu muda wa kuzoea ligi, Rupia yupo msimu wa tatu sasa nchini, ameizoea ligi na amekuwa mmoja wa wafungaji bora, nadhani atatu-

INAENDELEA UK. 23



Beki wa Timu ya Taifa ya Wavulana ya Tanzania ya umri chini ya miaka 15, Erick Yusuph (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Uganda katika mechi ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-15), iliyofanyika kwenye Uwanja wa St. Mary's Kitende, Uganda jana. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

## Yanga yakiri TP Mazembe wameshika hatima yao CAF

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI na wachezaji wa klabu ya Yanga umekiri kuwa mchezo wao ujao dhidi ya TP Mazembe ndio wenye hatima yao katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga inahitaji ushindi tu kujaribu kuweka hai matumaini yao ya kutinga hatua ya robo fainali na wachezaji wao wote wameanza maandalizi kuelekea kwenye mchezo huo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam Msemaji wa klabu hiyo, Ally Kamwe, alisema kila mchezaji morali ipo juu kuelekea mchezo huo na wote wameanza mazoezi isipokuwa beki wa pembeni Shadrack Boka ambaye bado anauguza majeraha.

"Kinachotupa moyo ni kuona wachezaji ambao walikuwa majeruhi wamerejea uwanja wa mazoezi, Aucho (Khalidy), Mzize (Clement) wote wameanza mazoezi, kila mchezaji anautaka huu mchezo kwa sababu wanajua ndio umebeba hatima yetu," alisema Kamwe.

Alisema maandalizi yote ya mchezo huo yanaendelea vizuri na wanatarajia kuondoka leo majira ya saa 5:00 asubuhi kuelekea Lubumbashi kukabiliana na wenyeji wao hao.

"Tunatarajia kuona idadi kubwa ya mashabiki wakielekea Lubumbashi, mpaka sasa nina idadi ya mashabiki zaidi ya 50 ambao wamekodi magari kwenda kuishangilia timu yao," alisema Kamwe.

Aidha, aliwataka mashabiki wengine kujikusanya na kuelekea Lubumbashi kwa ajili ya kuisapoti timu yao hiyo.

"Hapa nina taarifa kuna mashabiki wetu kutoka Zambia nao wataanza safari kwenda Lubumbashi, naamini idadi itaongezeka zaidi, na hawa ndio mashabiki wa Yanga, hata timu inapokuwa na matokeo mabaya bado wanakuwa nayo na kuisapoti, wanastahili kuwa mashabiki bora wa mwakani duniani," alisema.

Yanga itawakabili TP Mazembe ugenini, Jumamosi, ambapo mchezo huo unatarajiwa kuanza saa 10:00 jioni.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >